# SHERIA YA VYAMA VYA KISIASA: TOLEO LA UMMA-PROF CATHERINE NDUNGO

## YALIYOMO


SURA YA 1: UTANGULIZI ..... 1

Maana, kusudi na historia ya vyama vya kisiasa ..... 1

Historia ya chimbuko la vyama vya kisiasa nchini Kenya ..... 1

SURA YA 2: SHERIA NA MFUMO WA VYAMA VYA KISIASA NCHINI KENYA ..... 2

Sheria za Vyama vya Kisiasa ..... 3

Katiba ya Kenya 2010 ..... 3

Sheria ya Vyama vya Kisiasa ya mwaka wa 2011 ..... 4

Sheria ya Uchaguzi ya mwaka wa 2011 ..... 4

Sheria Zingine ..... 13

Mifumo ya Kitaasisi ya Kudhibiti Vyama vya Kisiasa ..... 14

Afisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa ..... 14

Kamati Patanishi ya Vyama vya Kisiasa ..... 17

Baraza ya Kutatua Mizozo ya Vyama vya Kisiasa ..... 17

SURA YA TATU: TARATIBU ZA KUUNDA NA KUSAJILI VYAMA VYA KISIASA ..... 19

Utaratibu wa kusajili vyama vya kisiasa ..... 19

Usajili wa muda ..... 19

Ombi la usajili wa muda ..... 19

Cheti cha usajili wa muda ..... 20

Haki za chama kinachosajiliwa kwa muda . ..... 20

Usajili kamili ..... 21

Ombi la usajili kamili ..... 21

Masharti ya usajili kamili ..... 21

Cheti cha usajili kamili ..... 22

Hadhi ya kishirika ya chama kilichosajiliwa kikamilifu ..... 22

SURA YA NNE: KUFUTA KWA USAJILI WA CHAMA CHA KISIASA ..... 22

Sababu za kufuta usajili wa chama ........ 22
Utaratibu wa kufuta usajili wa chama ........ 23
Matokeo ya kufutwa kwa usajili wa chama ........ 24
Kufunga shughuli za chama cha kisiasa ........ 24
Kusajiliwa tena kwa chama kilichopokonywa usajili ........ 24
Kufutwa kwa usajili kwa hiari ........ 25
Usajili kuahirishwa kwa muda ........ 25
Sababu za usajili kusitishwa kwa muda na matokeo yake ........ 25
Matokeo ya kuwekwa kando kwa muda ........ 25
SURA YA TANO: ANAYESTAHILI KUWA MWANACHAMA WA CHAMA CHA KISIASA ........ 25
Jinsi ya kuwa mwanachama ........ 25
Uandikishaji wa wanachama ........ 26
Kutokubaliwa kuwa na cheo katika chama cha siasa ........ 26
Haki za mwanachama ........ 26
Majukumu ya wanachama wa chama cha kisiasa ........ 26
Makundi maalumu ........ 27
Vizuizi kwa maafisa wa umma katika chama cha kisiasa ........ 27
Kanuni hizi hazihusiki na Rais, Makamu wa Rais, mbunge, gavana, naibu wa gavana ama mbunge wa bunge la kaunti ........ 27
Kutokubaliwa kuwa kiongozi katika chama cha kisiasa ........ 27
Kusitisha kuwa mwanachama wa chama cha kisiasa ........ 27
Kujiuzulu ........ 28
Kufukuzwa ........ 28
'Kuonekana' ........ 28
SURA YA SITA: KATIBA AMA KANUNI ZA CHAMA CHA KISIASA ........ 29
Mambo ambayo yapaswa kuzingatiwa katika katiba ama kanuni za chama ........ 29
SURA YA SABA: MIUNGANO NA MISETO ........ 32
Miungano ........ 32
Malengo ya vyama ya kuungana. ........ 32
Utaratibu wa kuomba muungano ........ 33
Uanachama wa chama cha muungano ........ 33
Athari za muungano ........ 33
Mseto ........ 34
Mikataba ya mseto ........ 34

Mkataba wa mseto lazima ueleze-: .......... 34
Aina za miseto .......... 35
Mseto wa kabla ya uchaguzi .......... 35
Mseto wa baada ya uchaguzi .......... 36
Matokeo ya kuunda mseto .......... 36
Kubadilisha mkataba wa mseto .......... 37
Kuvunja mseto .......... 37
SURA YA 8: MFUMO WA USIMAMIZI WA VYAMA VYA KISIASA .......... 37
Rekodi za chama cha kisiasa .......... 37
Afisi ya kaunti .......... 38
Ukaguzi wa rekodi za vyama vya kisiasa .......... 39
Mikutano ya umma ya chama cha kisiasa .......... 39
SURA YA 9: UTAWALA WA FEDHA .......... 39
Mahali ambapo fedha za vyama vya kisiasa hutoka .......... 40
Hazina ya Vyama vya Kisiasa .......... 40
Chanzo na sababu za kuwepo kwa hazina ya vyama vya kisiasa .......... 40
Malengo ya hazina .......... 41
Mahali fedha za hazina hii zinatoka .......... 41
Vizuizi vya kutumia fedha za Hazina .......... 42
Masharti ya kutimiza ili kupata mgao wa fedha za hazina ya vyama vya kisiasa .......... 43
Ugawaji wa fedha za hazina ya vyama vya kisiasa .......... 43
Vigezo vya kugawa fedha .......... 44
Makosa juu ya chanzo cha fedha .......... 44
Kuweka wazi habari za rasilimali, madeni na matumizi ya fedha katika shughuli za uchaguzi .......... 45
Ukaguzi wa akaunti za vyama vya kisiasa .......... 45
Akaunti na ukaguzi wa matumizi ya fedha katika Afisi ya Msajili .......... 46
Michango .......... 46
Aina za mchango .......... 46
Mchango wa kifedha .......... 46
Mchango usio wa kifedha .......... 46
Wanaofaa kuchangia .......... 46
Kukubali mchango .......... 47
Kiwango cha mchango .......... 47

Mchango usiofaa ........ 47
SURA YA 10: MAHITAJI YA KUTOA RIPOTI ........ 47
Ripoti ambayo haihusu fedha ........ 47
Mabadiliko ambayo sharti msajili wa vyama vya kisiasa afahamishwe ........ 47
Mabadiliko ya viongozi waliochaguliwa ........ 48
Notisi ya kubadilishwa kwa sehemu au anwani ya afisi za makao makuu ........ 48
Kuripoti kuhusu masuala ya fedha ........ 48
Baada ya kusajiliwa ........ 48
Ripoti ya kifedha ya kila mwaka ........ 49
Kuhusu uchaguzi ........ 49
Ukaguzi wa akaunti na matumizi ya fedha ........ 49
SURA YA KUMI NA MOJA: KANUNI ZA MAADILI ZA VYAMA VYA SIASA ........ 49
Matokeo ya kutozingatia kanuni za maadili ........ 52
Makosa na adhabu ........ 52

# SURA YA 1: UTANGULIZI

## Maana, kusudi na historia ya vyama vya kisiasa

Chama cha kisiasa ni muungano ama shirika la watu ambao wana nia ya kisiasa ya kugombea ama kusaidia wagombea wa uchaguzi wa kisiasa wa vyeo vya kitaifa na vya kaunti kwa lengo la kuwa na ushawishi wa kuunda serikali.

Jukumu la msingi la vyama vya kisiasa ni kuchangia ushiriki wa kidemokrasia kwa kuhamasisha umma kushiriki katika uchaguzi wa kisiasa kwa kuonyesha upendeleo wao kwa Raise, bunge na mabunge ya kaunti.

Vyama vya kisiasa pia huwa vyombo muhimu katika utungaji wa sera za umma, kuteua na kuchagua viongozi wa kisiasa

## Historia ya chimbuko la vyama vya kisiasa nchini Kenya

Baada ya majadiliano juu ya uhuru wa Kenya katika Kongamano la Lancaster la mwaka wa 1962, vyama viwili vya kisiasa Kenya African National Union (KANU) na Kenya African Democratic Union (KADU) viliundwa.Katika uchaguzi wa kitaifa uliofanywa mwezi wa Mei 1963, chama cha KANU kilishinda kwa wingi wa kura katika vyumba vyote viwili vya bunge. Chama cha KADU kilijivunja kwa hiari na kujiunga na chama cha KANU. Katika mwezi wa Machi mwaka wa 1964, Chama cha Kenya People's Union (KPU) kiliundwa baada ya tofauti za kiitikadi, migogoro ya uongozi na kutokubalika kwa maoni tofauti katika chama cha (KANU). Hata hivyo chama cha KPU kilipigwa marufuku mwaka wa 1969. Kiutekelezaji, Kenya ikawa nchi ya chama kimoja kutoka wakati huo hadi mwaka wa 1992 wakati katiba ilibadilishwa tarehe tisa Juni 1992 na kuifanya Kenya kuwa nchi ya Chama kimoja kisheria.Desemba mwaka 1991, bunge lilibadilisha kifungu cha 2A cha katiba ambacho kilifungua mlango wa Kenya kuwa na mfumo wa vyama vingi, hali ambayo ilitamatisha nafasi za pekee za KANU kuwa na mamlaka.

Kwa miaka mingi, hapakuwa na sheria maalum ya kudhibiti vyama vya kisiasa nchini Kenya. Vyama vya kisiasa vilisajiliwa na msajili wa vyama chini ya Sheria ya Vyama, kifungu cha 108. Sheria hii ndiyo ilitumika kusajili vyama vyote vikiwemo vya akina mama na vilabu vya mipira. Kwa hakika, vyama vya kisiasa vilikuwa miuungano ya kibinafsi. Nafasi ya kidemokrasia ya mwaka wa 1991 ilichangia kuongezeka kwa vyama ambavyo vilikuwa dhaifu na havikuwa na miundo misingi imara.

Ukosefu wa sheria mwafaka ya usajili, uendeshaji, udhibiti na ufadhili ulichangia kufanya vyama vya kisiasa kuwa mali ya watu binafsi na havikuwa na utambulisho wa kisheria na mpangilio wa ukuaji . Kimsingi, vyama vya kisiasa vilikuwa mali ya watu binafsi na baadhi ya watu waliunda

vyama vya kisiasa wakitegea kuviuza ili wapate faida kiuchumi.  Kwa hivyo hapakuwa na sheria ya kukuza mazingira ya kidemokrasia ya kuhusisha wananchi katika serikali.

Kati ya 1993-1994, bunge lilijaribu mara nne kupitisha sheria ya kipekee ambayo ingetumika katika kuendesha, usajili na ufadhili wa vyama vya kisiasa bila mafanikio.  Uhuru wa kuandikisha vyama vya kisiasa ulichangia katika uundaji wa vyama vingi ambavyo vilizozana, vikagawanyika na kusambaratika kwa vingine ili kuunda vyama vipya baadhi yake vikiwa na majina na/au ishara sawa.Kabla ya uchaguzi wa kitaifa wa mwaka 2007 kulikuwa na vyama 168 ambavyo vilikuwa vimesajiliwa na vyama mia moja na kumi na saba vilishiriki katika uchaguzi mkuu.  Ni katika muktadha huu ambapo sheria ya vyama vya kisiasa ilipitishwa katika mwaka wa 2007. Lengo la sheria hii ilikuwa ni kushughulikia usajili, udhibiti na ufadhili wa vyama.  Sheria hiyo ilianza kutumika tarehe moja mwezi wa saba mwaka wa 2008 na ofisi ya Msajili wa Vyama iliundwa. Vyama vyote vya kisiasa ambavyo vilikuwa vimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vilihitajika kujisajili upya kulingana na sheria mpya ya usajili wa vyama vya kisiasa kwa muda wa siku mia moja nathemanini (180).  Hali hii ilichangia kupungua kwa vyama kutoka mia moja sitini na nane (168) hadi arobaini na saba ( 47) katika mwaka wa 2009.

Katiba ya Kenya 2010 ilipopitishwa ilizua mwelekeo mpya katika udhibiti na utawala wa vyama vya kisiasa.  Katiba inatambua vyama vya kisiasa kama asasi muhimu katika kukuza demokrasia. Katiba, mbali na kuhakikishia kila mtu uhuru wa kuungana na wengine na hiari ya kuamua mwelekeo wa kisiasa pamoja na kulinda na kushiriki katika harakati za chama cha kisiasa, inabainisha mahitaji ya vyama vya kisiasa.  Vile vile inahitaji bunge litunge sheria ya kudhibiti hali mbalimbali za vyama vya kisiasa. (Tazama sura ifuatayo). Kwa mujibu wa mahitaji haya Katiba, Sheria ya Vyama vya Kisiasa 2011 ilitungwa.

## SURA YA 2:  SHERIA NA MFUMO WA VYAMA VYA KISIASA NCHINI KENYA

Sheria za kimsingi zinazodhibiti uundaji, usimamizi na utawala wa vyama vya kisiasa zimo katika Katiba ya Kenya 2010 pamoja na Sheria ya Vyama vya Kisiasa ya mwaka 2011. Hata hivyo, kuna sheria zingine ambazo zina athari katika uendeshaji wa vyama vya kisiasa. Hizi ni pamoja na Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2011, Sheria kuhusu Makosa katika Uchaguzi ya mwaka 2016, Sheria uhusu Ufadhili wa Kampeini za Uchaguzi ya mwaka wa 2013, Sheria kuhusu Ushirikiano na Utangamano wa Kitaifa ya mwaka wa 2008 pamoja na Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya mwaka wa 2011.

## Sheria za Vyama vya Kisiasa

### Katiba ya Kenya 2010

Katiba ya Kenya 2010, kama sheria kuu, inaweka msingi imara kisheria wa vyama vya kisiasa. Kuanzia mwanzo, katika utangulizi wake, Katiba inawathibitishia wananchi wa Kenya mamlaka na haki yao ya kipekee ambayo hawawezi wakanyimwa ya kuchagua muundo wa uongozi wa nchi mbali na kutambua matamanio yao kuhusu serikali iliyojengwa kwa msingi wa maadili u ya haki za binadamu, usawa, uhuru, demokrasia, haki za kijamii pamoja na utawala wa sheria.

Kifungu cha 4 cha Katiba ya Kenya, kinanaeleza kuwa Kenya ni nchi ya demokrasia ya vyama vingi iliyojengwa kwa msingi wa maadili ya kitaifa na kanuni za uongozi.

Kifungu cha 27 kinaitaka serikali kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa si zaidi ya thuluthi mbili ya viongozi waliochaguliwa au kuteuliwa katika nyadhifa mbalimbali za uongozi watakuwa watu wa jinsia moja.

Kifungu cha 38 kinatoa mwongozo wa haki za kisiasa na kumhakikishia kila mwananchi uhuru wa kufanya uamuzi wa kisiasa ikiwa ni pamoja na kuunda au kushiriki katika kuunda chama cha kisiasa, kushiriki katika shughuli za chama cha kisiasa, au kuwateua wanachama wa chama cha kisiasa na kukifanyia kampeni chama cha kisiasa.

Kifungu cha 91 pia kinaweka wazi mahitaji ya kimsingi kwa vyama vya kisiasa na kinafafanua kuwa vyama vya kisiasa havitafanya yafuatayo:

(a) kuundwa kwa misingi ya kidini, lugha, rangi, kabila, jinsia au kieneo ili kueneza chuki kwa njia yoyote ya aina hii;
(b) kujihusisha au kuchochea fujo na kuwatisha wanachama au wafuasi wake au wa wapinzani wake au mtu yeyote;
(c) kuunda au kuimarisha jeshi la wananchi, makundi ya kigaidi au makundi kama hayo;
(d) kutoa na kupokea hongo au kushiriki katika aina yoyote ya ufisadi; au
(e) kukubali au kutumia mali ya umma kuendeleza ajenda zake au za wagombea wake katika uchaguzi (isipokuwa pale ambapo imeruhusiwa kisheria).

Kifungu cha 92, kinalitaka bunge kutunga sheria ambayo itasimamia kampeni za uchaguzi, kanuni, majukumu na utendakazi na kuundwa na kusimamiwa kwa Hazina ya Vyama vya Kisiasa Mahitaji haya ya Kikatiba yamepewa nguvu ya utekelezaji kupitia Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2011, Sheria kuhusu Makosa katika Uchaguzi ya mwaka 2016, Sheria kuhusu Ufadhili wa Kampeni za Uchaguzi ya mwaka wa 2013, Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya mwaka wa 2011 na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2012.

### Sheria ya Vyama vya Kisiasa ya mwaka wa 2011

Sheria ya Vyama vya Kisiasa ilianza kufanya kazi mnamo tarehe moja mwezi wa Novemba mwaka wa 2011. Tangu kutungwa kwake, Sheria ya Vyama vya Kisiasa ya mwaka wa 2011 imefanyiwa marekebisho mara tatu kupitia sheria za bunge zifuatazo: Sheria ya Vyama vya Kisiasa nambari 18 (iliyofanyiwa marekebisho) ya mwaka wa 2014, Sheria ya Vyama vya Kisiasa nambari 21 (iliyofanyiwa marekebisho) ya mwaka wa 2014 na Sheria ya Vyama vya Kisiasa nambari 14 (iliyofanyiwa marekebisho) ya mwaka wa 2016

Sheria hii inatoa mwongozo wa:

(a) Shughuli ya usajili (mahitaji na masharti ya kusajiliwa kama mwanachama wa muda au mwanachama wa kudumu);
(b) Uanachama wa vyama vya kisiasa –kuzuiliwa kwa maafisa wa umma pamoja na vikwazo vya kushikilia wadhifa wa chama cha kisiasa, kujiuzulu;
(c) Ushirika wa vyama vilivyosajiliwa vya kisiasa;
(d) Miungano;
(e) Miseto ya Vyama;
(f) Kanuni na masuala yanayohusu vyama vya kisiasa;
(g) Rekodi za vyama vya kisiasa;
(h) Mikutano ya hadhara ya vyama vya kisiasa;
(i) Kufutiliwa mbali kwa vyama vya kisiasa na athari zake;
(j) Hazina ya vyama vya kisiasa;
(k) Maksudi na kugawanywa kwa fedha za hazina ya vyama vya kisiasa;
(l) Kuweka hesabu na kuchunguza matumizi ya hazina ya vyama vya kisiasa;
(m) Afisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa;
(n) Kamati ya kutatua mizozo ya vyama vya kisiasa;
(o) Kuvunjwa kwa vyama vya kisiasa;
(p) Makosa na adhabu ya jumla;
(q) Kanuni.

### Sheria ya Uchaguzi ya mwaka wa 2011

Sheria ya uchaguzi ya 2011 ndiyo sheria kuu inayosimamia uchaguzi nchini Kenya .Mambo muhimi yanayohusiana na vyama vya kisiasa katika Sheria hii ni;

**i) Uteuzi wa wagombea wa chama cha kisiasa**

Chama cha kisiasa kinahitajika kuwateuwa wagombea wake kwa ajili ya uchaguzi mkuu siku tisini kabla ya uchaguzi huo kwa mujibu wa katiba na kanuni zake. Katika uchaguzi mwingine ule, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka nchini inahitajika kutoa notisi, angalau siku 55 kabla ya uchaguzi huo ili kuonyesha siku ambayo chama kinapanga kuwateuwa wagombea wa urais, bunge la kitaifa au uchaguzi wa kaunti kulingana na katiba pamoja na kanuni za chama. Sheria hii inakizuia chama cha kisiasa kubadilisha jina la mwanachama aliyeteuliwa na jina lake kupokelewa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka nchini. Ikiwa mwanachama aliyeteuliwa atafariki, atajiuzulu au atashindwa kutekeleza majukumu yake au

atakiuka kanuni za maadili ya shughuli ya uchaguzi, basi chama kitamteua mwanchama mwingine baada ya kumfahamisha mwanachama husika kuhusu hatua ya kulibadilisha jina lake kabla ya siku yakuwasilisha karatasi zake za uteuzi kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka. Chama kinahitajika kusikiliza malalamishi ndani ya chama na kutatua mizozo hiyo kwa kipindi cha siku thelathini.

**ii) Uwasilishaji wa kanuni za uteuzi**

Chama cha kisiasa kinahitajika kuwasilisha kanuni zake za uteuzi kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka nchini angalau miezi sita kabla ya uteuzi wa wagombea. Baada ya kanuni hizo kupokelewa, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka nchini itapitia kanuni hizo katika kipindi cha siku kumi na nne ili kuhakikisha kuwa zinaambatana na miongozo iliyotolewa na hatimaye kutoa cheti cha kuthibitisha kuwa chama husika cha kisiasa kimetekeleza hatua hiyo ifaavyo au vinginevyo kukitaka chama hicho a kuhakikisha kuwa kinatekeleza masharti yafaayo kwa siku kumi na nne. Baadaye, Tume itatoa notisi kupitia Gazeti, yenye Kanuni zilizo na miongozi itakayofuatwa wakati wa uteuzi wa mchujo wa wagombea kwa kuzingatia kifungu cha 88 (4) (d) cha Katiba. Ikiwa Katiba haitafuatwa, basi kanuni hizo hazitazingtiwa AU zitakuwa batili. Mabadiliko yoyote ya kanuni za uteuzi wa mchujo huanza kutekelezwa siku tisini baada ya kupokelewa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka nchini.

**iii) Uwasilishaji wa orodha ya wanachama wa chama cha kisiasa**

Sharti chama cha kisiasa kinachomteua mtu kwa ajili ya uchaguzi kiwasilishe orodha ya wanachama wa chama chake kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.

(a) angalau siku mia moja na ishirini kabla ya siku ya uchaguzi huo, ikiwa ni uchaguzi mkuu; na

(b) angalau siku arobaini na tano kabla ya uchaguzi huo, ikiwa utakuwa uchaguzi mdogo.

Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka inatakiwa kuweka wazi kwa umma orodha ya majina ya wanachama wa vyama vyao.

**iv) Uteuzi wa maajenti**

Chama cha kisiasa kinaweza kumteua ajenti mmoja kwa kila kituo cha kupigia kura. Ikiwa chama hakitamteua ajenti kwa kituo cha kupigia kura, mgombea atamteua ajenti wake. Mgombea huru anaruhusiwa kumteua ajenti wake mwenyewe. Ikiwa ni kura ya maoni, kamati ya kura ya maoni iliyosajiliwa itamteua ajenti mmoja kwa kila kituo cha kupigia kura.

**v) Uteuzi wa wagombea wa viti mbalimbali vya uchaguzi katika chama**

Mtu yeyote anaweza kuchaguliwa kuwa mgombea wa wadhifa wa urais, ubunge au kiti chochote cha uchaguzi wa kaunti iwapo mtu huyo ameteuliwa kwa kuzingata Katiba au kanuni za chama husika chama kiidhinishe uteuzi huo kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka

Tume, iwapo itaombwa na chama, inaweza kuendesha na kusimamia uchaguzi wa mchujo wa wanaowania wadhifa wa urais, ubunge au chaguzi za kaunti . Ikiwa Tume itapokea maombi mengi ya kuandaa na kusimamia uchaguzi wa mchujo wa wagombea, Tume itaandaa na kusimamia uteuzi wa mchujo wa

wanaowania wadhifa wa urais, ubunge au chaguzi za kaunti; siku hiyo hiyo, katika kituo hicho hicho cha kupigia kura lakini katika vyumba tofautitofauti kwa kila chama kinachowasilisha wanachama wake. Bunge linafaa kutenga fedha zinazotakikana ili kuhakikisha kuwa Tume inakuwa na uwezo wa kuandaa na kusimamia uchaguzi huo. Kila chama cha kisiasa sharti kiwasilishe majina ya wagombea wa chama chake ambao wameteuliwa kushiriki katika uchaguzi huo angalau siku sitini kabla ya uchaguzi.

Angalau siku ishirini na moja kabla ya uchaguzi wa mchujo kufanyika, chama cha kisiasa kinahitajika kuikabidhi Tume majina ya wanachama wote wanaowania katika mchujo huo pamoja na siku ya uchaguzi wenyewe. Tume inahitajika kuchapisha kwenye Gazeti rasmi la serikali majina ya watu wanaowania uteuzi wa mchujo katika nyadhifa mbalimbali pamoja na tarehe ya uchaguzi huo katika kipindi cha siku saba baada ya kupokea majina ya wagombea.

Sharti anayewania wadhifa wa urais, ubunge au uchaguzi wa kaunti achaguliwe na wanachama wa chama chake cha kisiasa na jina lake liwe katika orodha ya majina yaliyokabidhiwa Tume.

Kila chama cha kisiasa kinahitajika kuifahamisha Tume kuhusu jina la mtu au watu ambao wamechaguliwa na mtu ama watu hao watahitahitajika kuwasilisha sampuli ya saini zao kama itakavyohitajika na Tume. Mtu huyu aliyeidhinishwa kwa niaba ya chama atathibitisha kuwa mgombea ameteuliwa na chama.

**vi) Orodha ya majina ya wagombea walioteuliwa**

Uteuzi wa wabunge wa Bunge la Kitaifa, Seneti na la kaunti kwa ajili ya kuunda orodha ya chama utakuwa kwa misingi ya uwakilishi.

Tume ilichapisha kanuni zinazofaa kutiliwa maanani wakati vyama vinaandaa orodha ya wanachama wake. Baada ya kupokea orodha ya chama, Tume huichunguza orodha hiyo ili kuhakikisha kuwa inaambatana na mwongozo uliotolewa na kisha huikabidhi chama cheti cha kuonesha kuwa kimezingatia masharti yote au hukitaka chama cha kisiasa kufanyia marekebisho orodha hiyo ili iambatane na Katiba la sivyo ikataliwe na Tume. Orodha ya chama iliyowasilishwa haitarekebishwa wakati wa kipindi cha bunge la kitaifa au la kaunti ikiwa patatokea na hali kama hiyo kwa wabunge waliokwisha kuteuliwa

. Mtu ambaye ameteuliwa na chama anatakiwa kuwa mwanachama wa chama hicho wakati wa kuwasilishwa kwa orodha ya majina ya wanachama wa chama. Orodha hiyo haitakuwa na jina la mgombea aliyeteuliwa kwa uchaguzi.

**vii) Uwasilishaji wa orodha ya wanachama**

Chama cha kisiasa kinahitajika kuwasilisha orodha ya wanachama kwa Tume angalau siku arobaini na tano kabla ya siku ya uchaguzi mkuu.

**viii) Ugawaji wa viti maalum**

Orodha ya wanachama wa chama itakayowasilishwa lazima iwe na;

a) Wanachama kumi na wawili walioteuliwa na vyama vya kisiasa vilivyo bungeni kwa mujibu wa idadi ya wanachama katika bunge la kitaifa ili wawe wawakilishi wa makundi maalumu wakiwemo vijana,watu wenye ulemavu na wafanyi kazi;

b) Wanawake kumi na sita walioteuliwa na vyama vya kisiasa kwa mujibu wa idadi ya wanachama wawakilishi katika bunge la seneti.

c) Wanachama wawili , mmoja wa kike na kiume ambao watawakilisha vijana ;

d) Wanachama wawili , mmoja wa kike na kiume ambao watawakilisha watu wenye ulemavu;

e) Idadi ya wanachama wanaohitajika ili kuhakikisha kuwa hapatakuwa na jinsia ambayo itakuwa na zaidi ya theluthi mbili katika bunge la kaunti; na

f) Idadi ya wanachama wa makundi yaliotengwa, wakiwemo watu wenye ulemavu na vijana..

Orodha ya majina ya chama yatakayowasilishwa katika makundi yaliyotajwa hapo juu sharti yawe na mfuatano wa wanawake na wanaume yakizingatia umuhimu wa jinsi yalivyoorodheshwa. Orodha ya chama ya wawakilishi ya waliotengwa lazima iwapatie kipaumbele mtu mwenye ulemavu, kijana na mwanachama ye yote yule atakayewakilisha kikundi cha waliotengwa.

Siku thelathini baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi mkuu, Tume huwateua wawakilishi kutoka kila orodha ya waliofuzu kwa mujibu ya uwakilishaji.

### ix) **Nafasi katika vyombo vya habari na wajibu wake**

Chama cha kisiasa kinachoshiriki katika uchaguzi kina haki ya kupata nafasi katika vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali wakati wa kampeni za uchaguzi.

### **x) Kanuni za maadili za uchaguzi**

Kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Uchaguzi, vyama vya kisiasa na mtu yeyote anayeshiriki katika uchaguzi au kura ya maoni anafaa kujua na kuzingatia Kanuni za Maadili ya Uchaguzi kama ilivyo katika kipengele cha pili cha Sheria hiyo.

Kanuni hizi zitatumika kwa kila chama cha kisiasa kinachoshiriki katika uchaguzi wa urais, ubunge, ugavana au uwakilishi wa wadi,kila mgombea ,kila kiongozi, kila ajenti mkuu na ajenti.

Lengo la Kanuni za Maadili katika Uchaguzi ni kuhakikisha kuwa pana mazingira yafaayo wakati wa uchaguzi yenye uwazi na haki pamoja na kuvumiliana katika shughuli za uchaguzi ambapo shughuli za kisiasa zitaendelea bila uoga, kushawishiwa visivyo, kutishwa au ulipizaji kisasi.

Vyama vyote vya kisiasa vilivyosajiliwa pamoja na wahusika wengine wanaoongozwa na kanuni hizi sharti wajitahidi kufanikisha malengo ya Kanuni hizi ili kuwezesha kampeini huru na mjadala wazi kwa umma ambao utafanyika kote nchini Kenya wakati wa uchaguzi. Vyama vilivyosajiliwa, kamati za kura ya maoni, maafisa wa vyama vya kisiasa na Kamati za kura ya maoni pamoja na wagombea wanaokubaliana na kanuni hizi, pia huwa wamethibitisha kuwa;

(a) watazingatia maadili na kanuni za Katiba;
(b) watahakikisha kuwa umma unafahamu kanuni hizi;
(c) watafanikisha kampeini za kuwahamasisha wananchi kuhusu upigaji kura;
(d) watakashifu, wataepuka na kuchukua hatua za kuzuia fujo na kuwatisha wengine;

(e) watawaelekeza na kuwafafanulia wagombea wao, viongozi maajenti, wanachama na wafuasi wengine wa chama hicho kuhusu kanuni hizi na yale wanayohitajika kufanya;
(f) watafanikisha usawa wa kijinsia;
(g) watawezesha kuvumiliana baina ya makabila;
(h) watakuza tamaduni mbalimbali;
(i) watawezesha uwakilishi sawa wa watu wenye mahitaji maalum;
(j) Kwa ujumla,watawahakikishia wahusika wote katika uchaguzi kuwa haki zao zitalindwa ili–
   (i) wajieleze na kusema maoni yao tofauti;
   (ii) wajadiliane na kushindana kwa misingi ya sera na miradi na ya vyama pinzani;
   (iii) watatafuta wanachama na kuomba kuungwa mkono na wapiga kura kwa njia huru;
   (iv) kufanya mikutano ya hadhara inayozingatia Sheria ya Taratibu za Umma (Sheria 56);
   (v) wahudhurie mikutano iliyoandaliwa na wengine;
   (vi) wasambaze maandishi na vifaa vya kampeni ambavyo haviudhi;
   (vii) wasichapishe na kusambaza matangazo ambayo waweke wapinzani wao;
   (viii) waweke mabango ambayo hayataudhi wengine;
   (ix) waondoe mabango yaliyowekwa wakati wa uchaguzi;
   (x) wafanikishe kampeini za uwazi kwa kuzingatia sheria zilizopo; na
   (xi) kushirikiana na Tume huru ya Uchaguzi na Mipaka na asasi husika za serikali pamoja na mamlaka nyingine iwayo katika kuchunguza masuala yanayoibuka wakati wa uchaguzi.

Wale wote wanaoongozwa na Kanuni hii wanahitajika, katika kipindi chote cha uchaguzi—

(a) kukashifu waziwazi na kila wakati fujo na vitisho, matumizi ya matusi, matamshi ya chuki au matumizi ya lugha inayoweza kusababisha fujo hata kama ni kwa kutaka kuonesha ubabe wa chama, kupata umaarufu fulani au kufaidi kwa njia yoyote ile;

(b) kuepuka visa vyovyote vya fujo au kutishana;

(c) kuhakikisha kuwa hakuna silaha za vita zinabebwa au kuonekana katika mikutano ya kisiasa au kuwepo katika maandamo au tukio linguine la kisiasa;

(d) kuepuka kufanya kampeini katika mazingira ya kuabudu au katika sherehe za mazishi;

(e) kushirikiana kwa nia nzuri na vyama vingine vya kisiasa ili kuepuka kuandaa mikutano ya kisiasa au maandamano katika sehemu moja kwa wakati mmoja;

(f) kutofanya chochote kuzuia haki za chama kingine,kupitia kwa wagombea wake, washauri au wawakilishi kuweza kuwafikia wapiga kura kwa ajili ya kuwaelimisha kuhusu upigaji kura, kufanya michango na kutafuta wafuasi;

(g) kuepuka kuiga alama, rangi na ufupisho wa majina ya vyama vingine, na kukataza na ikiwezekana kuzuia uondoaji, uumbuaji au kuharibu mabango ya kampeini ya vyama vingine;

(h) kuepuka kutoa au kuwapa watu wowote machapisho au zawadi wakiwataka watu hao wajiunge au wasijiunge na chama chochote wahudhurie mikutano yao, au wasihudhurie mikutano yoyote ya kisiasa ya wapinzani wao, wasipige kura au wakipiga basi wafanye hivyo kwa namna fulani; kukubali, kukataa au kuondoa jina la mgombea katika uchaguzi kwenye orodha ya wagombea wengine;

(i) kuepuka kujaribu kuitumia nafasi yake ya mamlaka au uwezo wa kushawishi vibaya ikiwa ni pamoja na uwezo wa mzazi, wa mume, wa kiserikali au mamlaka ya utamaduni wa kijamii kwa ajili ya siasa ikiwa ni pamoja na kutoa zawadi au kuwatishia;

(j) kuepuka ubaguzi wowote wa rangi, kijinsia, wa ujauzito, wa kindoa, kiafya, kikabila, kijamii, kiumri, ulemavu, kidini, kimawazo, kiimani, kitamaduni, kimavazi, lugha au wa ulikozaliwa kuhusiana na shughuli za uchaguzi au za kisiasa;

(k) Kuhusu Tume,

  (i) wataheshimu mamlaka ya Tume wakati wa shughuli za uchaguzi au upigaji kura ya maoni;

  (ii) kuhakikisha kuwa wawakilishi wanahudhuria na kushiriki katika mikutano yoyote ya kamati ya upatanisho pamoja na mikutano mingine itakayoandaliwa kwa niaba ya Tume;

  (iii) kutekeleza amri na maagizo ya Tume;

  (iv) kuisaidia Tume kupata nafasi ya kuwafikia maafisa wa uangalizi pamoja na wawakilishi wengine ili wahudhurie mikutano ya hadhara ya vyama vya kisiasa pamoja na shughuli zingine za uchaguzi;

  (v) watashirikiana na maafisa wengine wakati wa kufanya uchunguzi wa masuala na madai mengine yanayohusu shughuli za uchaguzi;

  (vi) watachukua hatua zifaazo ili kuhakikisha kuwa waangalizi pamoja na wawakilishi wengine wa Tume wamelindwa dhidi ya vitisho au kupigwa wakati wa kuendesha shughuli rasmi za Tume;

  (vii) kuanzisha na kuhakikisha kuwa pana njia faafu ya mawasiliano baina yao na Tume; na

  (viii) kutii yote yaliyomo kwenye Sheria hii;

(l) kuwahakikishia wapiga kura kuwa Tume haitaupendelea upande wowote na kwamba usiri na maadili ya upigaji kura yatazingatiwa ili kuyahakikishia kuwa hakuna anayefahamu namna mwenzake alivyopiga kura;

(m) kuchukua hatua zifaazo ili kuwaadhibu maafisa, wafanyakazi, wagombea au wafuasi wa chama cha kisiasa ambao—

  (i) watakiuka yaliyomo kwenye Sheria hii;

  (ii) watahusika katika visa, kwa kujua au kwa kutojua, ambavyo vinakiuka yaliyomo katika sheria za uchaguzi; na

(iii) wanakiuka au wanashindwa kuzingatia yaliyomo kwenye sheria za uchaguzi;

(n) kukubali kwamba maafisa, wafanyakazi, wagombea na wafuasi wa chama cha kisiasa taratibu za kunidhamishwa za Tume kutokana na ukiukaji wowote wa yaliyomo kwenye Sheria hii; na

(o) bila kuingilia haki ya kuwasilisha malalamishi katika mahakama, akubali matokeo ya uchaguzi na tangazo la Tume la matokeo hayo na vyeti vitakavyotolewa.

Ikiwa kulingana na Tume, chama cha kisiasa au kamati ya kura ya maoni itakiuka vipengele vya Kanuni hii, Tume inaweza kutoa adhabu mojawapo au zaidi miongoni mwa hizi ambayo itaondolewa tu kwa masharti yafuatayo—

(i) onyo kupitia barua rasmi;

(ii) faini itakayowekwa na Tume;

(iii) bila kujali sheria zingine zilizotungwa, amri ya kukizuia chama cha kisiasa,labda kwa kipindi chochote au kwa muda tu,kutumia vyombo vya habari kama vile televisheni au redio vilivyopo na vinavyotumiwa wakati wa uchaguzi;

(iv) amri ya kukizuia chama cha kisiasa, kamati ya kura ya maoni au mgombea —

(a) kuandaa mkutano wa hadhara, maandamano au mkutano wa aina yoyote ile;

(b) kuingia katika eneo lolote za kupigia kura kwa lengo la kutaka kuwashawishi wapiga kura au kwa nia yoyote ile ya uchaguzi;

(c) kuweka mabango au kuchapisha na kusambaza maandishi ya kampeini za uchaguzi;

(d) kuchapisha na kusambaza maandishi ya kampeni pamoja na kutoa matangazo ya uchaguzi au kupunguza nguvu za vyama vya kisiasa za kufanya hivyo na maafisa wote watafahamishwa kuhusu hatua hii kuwazuia kufanya hivyo chini ya Kifungu cha 56 cha Sheria ya uwajibikaji katika maeneo ya umma. Hatua hiyo itachukuliwa katika maeneo yatakayoathirika kwa mujibu wa Sheria hii.

(e) kuhusu kiongozi, mgombea, afisa au mwanachama wa chama cha kisiasa ambaye anaunga mkonochama cha kisiasa kamati ya kura ya maoni Tume itaweka mojawapo au zaidi ya adhabu au vikwazo ;

Faini itakayodaiwa na Tume kwa kuzingatia kanuni itasajiliwa Mahakama ya juu. Tume kwa kutumia mjadala wake au ripoti iliowasilishwa kwake, inaweza kuanzisha kesi katika Mahakama ya juu ifaavyo ikiwa Sheria hii itakiukwa na chama cha kisiasa, mgombea, afisa wa chama, mwanachama au mfuasi wa chama na pale mahakama itathibitisha ukiukaji wa sheria:

(a) ikiwa ni chama cha kisiasa, kutowajibika kutakakohusisha visa vyovyote vya kusababisha vurugu, kutishwa au kuvunjwa kwa haki za chama chochote cha kisiasa, mgombea au mpiga kura, mahakama inaweza mbali na kuongeza au kubadilisha adhabu na vikwazo vyo vyote, inaweza kufutilia mbali haki za chama husika kushiriki katika uchaguzi husika;

(b) ikiwa kiongozi, afisa aliye mamlakani, mwanachama au chama cha kisiasa, wafuasi wa chama au mgombea atakiuka sheria hiyo ikiwa ni pamoja na kuzua fujo au kutisha au kukiuka haki za kimsingi za chama kingine cha kisiasa, mgombea wa chama hicho au mpiga kura wake, mahakama itatoa adhabu ya kuhakikisha kuwa inamfutilia mbali mgombea husika na kumyima nafasi ya kuwania katika uchaguzi wowote au inaweza kufuta jina la mgombea huyo kutoka kwa orodha ya wagombea wanaohusika..

Wakati wa kufanya uamuzi wake kuhusu adhabu itakayotolewa, Tume au mahakama kuu, kulingana na hali itakavyokuwa, itaheshimu athari zingine za kisheria ambazo zinaweza kutokana na hatia za kijamii au za kiuhalifu na ambazo zitatokea kwa msingi wa makosa yaliyotajwa. Mahakama ya Juu itahakikisha kuwa mashtaka yote yaliyoanzishwa yanapewa kipaumbele na kushughulikiwa kabla ya matakwa mengine yaliyowasilishwa mbele ya Mahakama hiyo na kwamba maamuzi ya Mahakam hiyo yanatolewa kabla ya siku ya uchaguzi husika kufanyika. Shughuli ya Mahakama ya Juu kwa kuzingatia kesi zinazohusu Sheria hii zitakuwa kwa mujibu wa kanuni na mwongozo ambao utakuwa ukiidhinishwa mara kwa mara na Jaji Mkuu.

Kila chama cha kisiasa, kamati ya kura ya maoni mgombea au ajenti—

(a) wataheshimu majukumu ya wanahabari kabla, wakati na baada ya uchaguzi au kura ya maoni kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) hawatawazui wanahabari kuhudhuria mikutano ya kisiasa, maandamano na mikutano ya kampeni; na

(c) watachukua hatua zifaazo ili kuhakikisha kuwa wanahabari hawanyanyaswi, hawatishwikuwa hatarini au kupigwa na kuumizwa kwa njia yoyote na wawakilishi au wafuasi wa mgombea au chama cha kisiasa.

Kila chombo cha habari na wawakilishi wake watahitajika—

(a) kuzingatia kanuni za maadili ya kitaaluma ya wanahabari wakati wanapokusanya na kutangaza habari zinazohusu mikutano ya hadhara, mikutano ya kampeini za uchaguzi na maandano;

(b) kutochapisha wala kutangaza matokeo ya uchaguzi au kura ya wanaotoka kwenye kituo cha kupiga kura wakati upigaji kura au kura ya maoni inaendelea;

(c) kuzingatia mwongozo wowote wa uanahabari ambao utatolewa na Tume; na

(d) kuzingatia yaliyomo kwenye Sheria hii.

Tume itaunda Kamati ya Utekelezaji wa Kanuni za Maadili ya Uchaguzi. Kamati hii itakuwa na wanachama wasiopungua watano kutoka kwenye Tume ikiongozwa na mwenyekiti atakayeteuliwa na Mwenyekiti wa Tume. Tume inaweza kumteua mfanyikazi mmoja kutoka kwa ofisi yao kuwa katibu wa kamati hiyo. Mwenyekiti wa kamati hiyo atakuwa mtu ambaye ana uwezo wa kuwa jaji wa Mahakama ya Juu.

Kila mgombea, afisa au ajenti —

(a) ataheshimu mamalaka ya kamati ya kuhakikisha utekelezaji wa Kanuni hizi kwa niaba ya Tume;

(b) atahakikisha kuwa ametii amri zote zinazotolewa na kamati hiyo kwa vyama, wagombea na wawakilishi wake;

(c) atashirikiana na maafisa wa kamati katika kuchunguza madai yoyote yanayoibuliwa wakati wa uchaguzi; na

(d) ataheshimu na kutii kanuni zote za Kamati.

Kila chama kilichosajiliwa, kamati ya kura ya maoni wagombea na maajenti watahakikisha kuwa—

(a) wanawake na watu wanaoishi na ulemavu wanashiriki kwenye uchaguzi katika mazingira yaliyo na usalama;

(b) wanaheshimu haki za wanawake na kuwaruhusu kujieleza katika vyama vya kisiasa, kamati husika na kwa wagombea wengine;

(c) wanawake wanashiriki kwa usawa na kwa ukamilifu katika shughuli za kisiasa;

(d) wanawake na watu wanaoishi na ulemavu wamepata fursa ya kuhudhuria mikutano ya kisiasa, maandamano au shughuli nyinginezo za chama; na

(e) wamechukua hatua zifaazo ili wanawake washiriki kwa uwazi katika shughuli zozote za kisiasa.

Tume inaweza kubuni kamati za amani katika kila eneo bunge wakati wa uchaguzi au wakati wa kura ya kuifanyia katiba marekebisho.

Kila chama cha kisiasa, kamati ya kuifanyia katiba marekebisho, mgombea, afisa au ajenti atahakikisha kuwa—

(a) anatambua shughuli za kamati ya amani itakayokuwa imeundwa na Tume katika eneo bunge;

(b) anahudhuria mikutano ya kamati ya amani iliyoitishwa katika eneo bunge kwa niaba ya Tume; na

(c) anahusika katika jopo la uchunguzi litakaloundwa na kamati ya amani kuhusu masuala yanayotokana na uchaguzi.

Kamati ya amani ina mamlaka ya—

(a) kuvipatanisha vyama vinavyozozana;

(b) kutatua mizozo ya kisiasa katika kiwango cha eneo bunge;

(c) kushirikiana na vyombo vya usalama serikalini na kuripoti visa vyovyote wakati wa uchaguzi katika eneo bunge; na

(d) kuripoti ukiukaji wowote wa Sheria za uchaguzi kwa kamati hii ili hatua mwafaka zichukuliwe.

Sheria inatumika—

(a) wakati wa uchaguzi mkuu, kuanzia siku ambapo notisi ya kuandaliwa kwa uchaguzi huo itatolewa hadi siku ambapo viongozi walioteuliwa wataapishwa; na

(b) wakati wa uchaguzi mdogo, kuanzia wakati kiti husika kinatangazwa kuwa wazi hadi wakati ambapo viongozi wateule wataapishwa.

Mtu yeyote anaweza kulalamika kuhusu ukiukaji wa Sheria hii.

### Sheria Zingine

**Sheria kuhusu Makosa ya Uchaguzi ya mwaka 2016**,

Sababu kuu ya Sheria kuhusu Makosa ya Uchaguzi ya mwaka 2016 ni kutoa mwongozo juu ya hatia wakati wa uchaguzi na mambo yanayoyohusiana nao. Kuhusu vyama vya kisiasa Sheria inabainisha haya kuwa hatia:

(a) mtu ye yote kutoa hongo, kutumia ushawihi usiostahili, kumlazimisha au kutumia vyombo vya usalama wa kitaifa kumfanya mtu huyo kukipigia chama chochote kura.

(b) maafisa wa umma kushiriki katika shughuli za kisiasa au kutumia mali ya umma kuunga mkono chama chochote cha kisiasa.

(c) afisa ye yote wa chama cha kisiasa kujaribu kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchaguzi bila kuzingatia kanuni za maadili ya uchaguzi.

**Sheria ya Ufadhili wa Kampeni za Uchaguzi ya mwaka wa 2013**

Sheria hii inalenga kudhibiti mchango, msaada na matumizi ya fedha wakati vyama vya kisiasa vinafanya kampeni za uchaguzi. Sheria hiyo iliacha kufanya kazi hadi baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2017. Sheria hiyo inaipa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka jukumu la:

(a) kuhifadhi rejesta ya watu walioruhusiwa ;
(b) kuchunguza wagombea, vyama vya kisiasa, kamati ya kusimamia upigaji kura ya maoni pamoja na watu walioruhusiwa kushughulikia matumizi ya fedha za kampeni;
(c) kuweka kiwango cha matumizi ya fedha za kampeni na kuhakikisha kuwa viwango hivyo vinazingatiwa;
(d) kuweka viwango na kuthibitisha unakotoka mchango wa mgombea, chama cha kisiasa au wa kamati ya maoni ;
(e) kuchunguza na kudhibiti matumizi ya fedha katika kampeini;
(f) kutoa mwongozo wa kuripoti matumizi ya fedha za kampeni;
(g) kutoa ushauri kwa mgombea, chama cha kisiasa au kamati ya kura ya maoni kuhusu masuala yoyote yanayohusu matumizi ya fedha za kampeni; na
(h) kutoa mwongozo na kuhakikisha kuwa mwongozo huo unatekelezwa kwa ajili ya kudhibiti vyombo vya habari;
(i) kutekeleza majukumu mengineyo ambayo yanaweza kuwa muhimu kwa makusudio ya sheria hii.

Isitoshe, sheria hii inavitaka vyama vya kisiasa ambavyo vinataka kushiriki katika uchaguzi kuunda kamati ya chama inayosimamia matumizi ya fedha ili iweze:

(a) kufungua akaunti ya kamati ya chama inayosimamia matumizi ya fedha ambapo kutawekwa fedha zote ya kampeni ya uchaguzi;
(b) kuwa mojawapo wa wale wanaotakiwa kutia sahihi ili kuidhinisha matumizi ya fedha za akaunti ya kamati ya chama inayosimamia matumizi ya fedha;
(c) kutoa ushauri kwa vyama vya kisiasa kuhusu masuala yote yanayohusu fedha kwa ajili ya uteuzi wa wanachama au matumizi ya fedha za kampeni;
(d) kusimamia akaunti ya kamati ya chama inayosimamia matumizi ya fedha na kuhakikisha kuwa vitabu vya hesabu na rekodi nzuri ya fedha imewekwa mbali na kuhakikisha kuwa rekodi hizo zinaweza kuchunguzwa wakati wowote;
(e) kupokea ripoti ya matumizi ya fedha za uchaguzi wa mchujo pamoja na matumizi ya fedha za kampeni ya kila mgombea;
(f) kuchunguza matumizi ya fedha za kampeni kwa kila mgombea ili kuhakikisha kuwa wagombea hawa wanatimiza masharti ya matumizi ya fedha wakati wa kampeni za uchaguzi wa mchujo;
(g) kuweka pamoja ripoti za matumizi ya fedha zilizopokelewa kutoka kwa wagombea wa chama na kisha kuziwasilisha kwa Tume ripoti ya awali ya kampeni za uchaguzi wa mchujo na ripoti ya mwisho ya shughuli hiyo; na
(h) kuwasilisha kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ripoti ya mwisho ya matumizi ya fedha za kampeni za uchaguzi wa mchujo wa chama cha kisiasa.

**Sheria ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa ya mwaka wa 2008**

Sheria hii inahimiza umoja na utangamano wa kitaifa kwa kupinga:

(a) ubaguzi kwa misingi ya kikabila;
(b) kubaguliwa kwa kuonewa;
(c) kudhulumiwa kwa misingi ya ukabila;
(d) ubaguzi katika ajira;
(e) ubaguzi wa uanachama katika miungano;
(f) kubaguliwa na mashirika;
(g) ubaguzi katika kupatikana na kugawiwa rasilimali za umma;
(h) ubaguzi katika umiliki, usimamizi na uuzaji wa mali; na
(i) matamshi ya chuki.

## Mifumo ya Kitaasisi ya Kudhibiti Vyama vya Kisiasa

### Afisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa

Sheria inaidhinisha kuwepo kwa afisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa. Afisi hii hutekeleza sheria hii ikiongozwa na Msajili wa Vyama vya Kisiasa (Msajili). Msajili husaidiwa na manaibu watatu ambao mmoja wao sharti awe wa jinsia tofauti. Afisi ya Msajili inaweza kuwaajiri kwa muda wafanyakazi, wataalamu au washauri kwa ajili ya utendakazi na utekelezaji wa shughuli za afisi hiyo kulingana na Sheria ya Vyama vya Kisiasa au sheria yoyote iliyoandikwa. Yeyote

atakayehudumu kama Msajili au naibu wa msajili hafai kuwania wadhifa wowote wa kisiasa kama vile ubunge wa bunge la kitaifa au la kaunti au hata wa kuwa mwanachama wa kamati ya uongozi wa chama chochote cha kisiasa katika kipindi cha miaka mitano baada ya kuacha kuhudumu katika nafasi hiyo.

Msajili wa vyama vya kisiasa kwa ujumla husajili, hudhibiti, huchunguza na kusimamia vyama vya kisiasa ili kuhakikisha kuwa vinatimiza matakwa ya Sheria ya Vyama Vya Kisiasa.

Majukumu mengine ni pamoja na:

(a) kusimamia Hazina ya Vyama vya Kisiasa;

(b) kushirikiana na wanachama wa Kamati Patanishi ya Vyama vya Kisiasa;

(c) kuhakikisha kuwa anachapisha ripoti ya kila mwaka kuhusu matumizi ya fedha za vyama;

(d) kuhifadhi sajili na alama za vyama vya kisiasa;
(e) kuhakikisha na kuthibitisha kuwa hakuna yeyote ambaye ni mwanachama wa vyama viwili tofauti vya kisiasa; na
(f) kufanya uchunguzi kuhusu malalamishi yanayopokelewa kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Kisiasa ya mwaka wa 2011.

### *Masharti ya kuhudumu kwa Msajili na Naibu*

Msajili na Naibu watahudumu kwa kipindi kimoja tu cha miaka sita na hawataruhusiwa kuteuliwa tena kwa awamu nyingine.

### *Nafasi ya Msajili au Naibu wa Vyama vya Kisiasa*

Kila panapotekea pengo katika afisi ya Msajili au Naibu, Raisi atamteua Msajili au naibu kutoka kwa orodha ya watu sita walioteuliwa na Tume ya Huduma za Umma na kutumwa kwa Rais kulingana na kipengele cha sita cha katiba. Hatimaye afisa huyo ataidhinishwa na bunge la kitaifa.

### *Kuondolewa afisini kwa Msajili au Naibu*

Msajili au Naibu anaweza kuondolewa afisini kwa madai yafuatayo-

(a) Ukiukaji mkubwa wa Katiba au sheria zilizopo;
(b) kushindwa kutimiza sura ya sita ya Katiba;
(c) ikiwa atashindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na upungufu wa akili au majeraha ya kimwili;
(d) kufilisika;
(e) ukosefu wa ujuzi unaohitajika; au
(f) Utovu wa nidhamu wa hali ya juu

***Hatua za kumwondoa Msajili au Naibu ofisini***

Yeyote anayetaka kumwondoa Msajili au Naibu ofisini, anahitajika kuwasilisha ombi (katika maandishi) la kufanya hivyo kwa Tume ya Huduma za Umma, huku akionyesha ushahidi wa kutosha wa kutaka kumwondoa Msajili au Naibu.

, Tume ya Huduma za Umma itaiangalia ombi hilo na ikiwa kuna ushahidi wa kutosha kumwondoa Msajili au Naibu afisini basi Tume itawasilisha ombi hilo kwa Rais.

Baada ya kulipokea na kulichunguza ombi hilo, Rais anaweza kumsimamisha kazi kwa muda Msajili au naibu huku akisubiri matokeo ya ombi hilo na aunde kamati ya kuchunguza suala hilo kulingana ambalo litatoa pendekezo la hatua itakayochukuliwa,

Kamati hiyo maalum ya uchunguzi itajumuisha—

(a) Mwenyekiti ambaye ameteuliwa na Tume ya Huduma ya Mahakama na ambaye anafaa kuhudumu kama jaji wa mahakama ya ngazi ya juu;

(b) Watu wengine wawili, mwanaume na mwanamke, watateuliwa na Chama cha Mawakili nchini na ambao wanafuzu kuwa majaji wa mahakama ya ngazi ya juu;

(c) Watu wawili, mwanamume na mwanamke ambao watateuliwa na Shirikisho la Vyama vya Wataalamu katika Afrika Mashariki na ambao wana maarifa na ujuzi katika masuala ya umma na wana uwezo wa kupata habari kuhusu suala husika la kuondolewa kwa afisa huyo.

Kamati maalum ya uchunguzi inahitajika kufanya uchunguzi wa suala hilo kwa haraka, iandae ripoti kuhusu ushahidi wa suala hilo na kumpa Rais mapendekezo yafaayo. Baadaye, Rais atachukua hatua sawa na mapendekezo ya ripoti hiyo kabla ya muda wa siku 30 kuisha. Afisa ambaye ataachishwa kazi kwa kuzingatia utaratibu huu ataendelea kupokea nusu ya mshahara wake pamoja na marupurupu yanayotokana na wadhifa wake.

***Vigezo vya kutimiza ili kuteuliwa kuwa Msajili au Naibu***

Yeyote anafuzu kuteuliwa kuwa Msajili au Naibu ikiwa ana shahada kutoka chuo kikuu chochote kinachofahamika nchini Kenya,na maarifa ya kutosha na ujuzi wa siku nyingi katika masuala yanayohusu fedha,usimamizi, sayansi ya kisiasa,sheria,uongozi au utawala wa umma.

Kuwa Msajili, mtu huyo lazima awe na tajriba au uzoefu wa kutosha katika eneo husika wa angalau miaka kumi na mitano tangu alipomaliza masomo yake ya chuo kikuu, na kwa yule anayetaka kuwa Naibu wa Msajili, lazima awe na tajriba au uzoefu wa kutosha katika eneo husika wa angalau miaka kumi tangu alipomaliza masomo yake ya chuo kikuu.

Watu hao wastahili kuwa watu wenye sifa nzuri na wadilifu mbali na kutimiza matakwa ya sura ya sita ya Katiba.

### *Kufutiliwa mbali kwa uteuzi wa Msajili au Naibu*

Mtu yeyote hastahili kuteuliwa kwa wadhifa wa Msajili au Naibu wa Vyama vya Kisiasa ikiwa amewahi kuwania wadhifa wa ubunge katika bunge la kitaifa au la kaunti au hata amewahi kuwa kiongozi wa chama cha kisiasa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kabla ya kuomba kazi katika nafasi hiyo .

### *Kiapo cha Kutwaa Uongozi*

Msajili na Naibu wa vyama vya kisiasa wanatakiwa kuapishwa kabla ya kuchukua hatamu za uongozi.

### Kamati Patanishi ya Vyama vya Kisiasa

Sheria ya Vyama vya Kisiasa inaidhinisha kuundwa kwa Kamati Patanishi ya Vyama katika kiwango cha kitaifa na kaunti. Lengo la kamati hii ni kutoa nafasi ya mazungumzo baina ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka pamoja na Vyama vya Kisiasa. Majukumu ya kamati hiyo pia yanasisitizwa katika Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya mwaka wa 2011 pamoja na Sheria ya Uchaguzi ya mwaka wa 2011 pamoja na Kanuni ya Maadili ya Uchaguzi .Kanuni za Maadili ya Uchaguzi zinavitaka vyama vya kisiasa kuhudhuria na kushiriki katika mikutano ya Kamati Patanishi ya Vyama vya Kisiasa.

### Baraza ya Kutatua Mizozo ya Vyama vya Kisiasa

Katika siku zilizopita, mizozo katika na baina ya Vyama vya Kisiasa imekuwa ikipelekwa mahakamani. Licha ya kuwa mahakama zilikuwa zikitoa uamuzi uliopendelewa sana na wahusika, kwa kiwango fulani zilisababisha masuala muhimu ambayo yalihitaji kushughulikiwa vyema na wanasiasa kutatuliwa na mahakimu. Zaidi ya yote, ililemaza maamuzi yaliyokuwa yakifanywa na vyama vya kisiasa na wakati mwingine kutishia uhuru wa mahakama.

Ili kurejesha nguvu za maamuzi ya kisiasa kwa Vyama vya Kisiasa, sheria hii inavitaka Vyama vya Kisiasa kuunda katiba yake na mbinu za ndani za kutatua mizozo. Mizozo ya ndani inayopatikana na uteuzi wa mchujo itashughulikiwa kwanza na vyama vyenyewe.

Vyama vinaweza kuitisha tu msaada wa kamati ya kutatua mizozo baada ya mbinu zote za ndani za kutatua mizozo hiyo kushindwa kufaulu. Kamati hii ya kutatua mizozo ya Vyama vya Kisiasa pia inajishughulisha na mizozo baina ya Vyama vya Kisiasa. Sheria hii inatoa mwelekeo wa kuunda Kamati ya Kutatua Mizozo ya Vyama vya Kisiasa. Kamati hii ina wanachama wafuatao ambao huwa wameteuliwa na Tume ya Huduma za Mahakama—

(a) Mwenyekiti ambaye anastahiki kuteuliwa kuwa jaji wa Mahakama ya Juu; na

(b) Wanachama wengine sita ambao watatu miongoni mwao ni mawakili wa Mahakama ya Juu wenye ujuzi wa kipekee wa miaka saba na watatu ni wenye ujuzi katika masuala ya uongozi, kiutawala, kijamii, kisiasa, kiuchumi miongoni mwa ujuzi mwingine muhimu.

Ili mkutano wa Baraza ufanyike, utahitaji kwa na watu watatu, mmoja wao lazima awe jaji wa mahakama ya juu.

Afisa yeyote wa umma au mtu anayejihusisha na shughuli za chama cha kisasa hafai kuteuliwa kuhudumu kama mwanachama wa Baraza hili. Vil evile mtu yeyote haruhusiwi kuhudumu katika Baraza hili ikiwa hajatimiza mahitaji ya Sura ya Sita ya Katiba.

Mwenyekiti na wanachama wa kamati hiyo hawatakuwa wafanyakazi wa kudumu. Mwenyekiti na wanachama watahudumu kwa kipindi cha miaka sita ambacho hakitaongezwa tena.

### *Majukumu ya Baraza la Kutatua Mizozo*

Majukumu ya Baraza la Kutatua Mizozo ya Vyama vya Kisiasa ni:

(a) kutatua mizozo baina ya wanachama wa chama fulani;

(b) kutatua mizozo baina ya mwanachama na chama chake cha kisiasa;

(c) kutatua mizozo baina ya vyama vya kisiasa;

(d) kutatua mizozo baina ya mgombea huru na chama cha kisiasa;

(e) kutatua mizozo baina ya vyama  vya muungano wa kisiasa;

(f) kusikiza rufaa za  uamuzi wa Msajili kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Kisiasa; na

(g) kutatua mizozo kutokana na uchaguzi wa mchujo katika vyama.

Baraza la kutatua mizozo halina ruhusa ya kusikiliza au kutatua mizozo kati ya wanachama na chama cha kisiasa, kati ya vyama vya kisiasa ama kati ya mgombea huru na chama cha kisiasa isipokuwa pale ambapo mzozo huo uwe umesikilizwa na kuamuliwa na kamati ya kutatua mizozo ya chama husika cha kisiasa.

### *Uamuzi wa Mizozo*

Baraza la kutatua mizozo lihitajika kutoa uamuzi wa mzozo utakaowasilishwa kwake kwa kipindi cha miezi mitatu tangu kuwasilishwa kwa malalamishi. Kesi ya rufaa itakayowasilishwa katika Mahakama ya Juu itatokana na uamuzi wa Baraza hilo kwa misingi ya sheria na ukweli pamoja na misingi ya Sheria ya Mahakama ya Rufaa na Mahakama ya Upeo .Uamuzi wa Baraza la Kutatua Mizozo ya Kisiasa hutekelezwa sawa na namna uamuzi mwingine wa mahakama hutekelezwa.

### *Kuondolewa kwa mwanachama wa Baraza.*

Tume ya Huduma za Mahakama inaweza kumwondoa mwanachama wa Baraza ikiwa mwanachama huyo atafilisika,atahukumiwa kwa uhalifu,atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa muda mrefu kutokana na majeraha ya kimwili au  akili,kutenda kinyume na Katiba ama kwa vyo vyote  vile, hana uwezo wa kutekeleza majukumu yake.

### *Wafanyakazi wa Baraza*

Tume ya Huduma za Mahakama ina jukumu la kumteua Katibu pamoja na maafisa wengine wa Baraza ili kufanikisha utendakazi wa Baraza.

### *Matumizi ya fedha ya Baraza*

Mishahara ya wafanyakazi na matumizi ya Baraza hulipwa kutokana na pesa zilizotengwa na Bunge la Taifa kwa ajili ya Hazina ya Mahakama. Mwenyekiti na wanachama wa Baraza hulipwa marupurupu pamoja na pesa za matumizi kwa mujibu wa mwongozo wa Tume ya Huduma za Mahakama kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Kushughulikia Mishahara na Malipo.

## SURA YA TATU: TARATIBU ZA KUUNDA NA KUSAJILI VYAMA VYA KISIASA

Kikundi cha watu wenye umri wa miaka 18 na zaidi ama shirika ambalo lina nia ya kuendesha shughuli zake kama chama cha kisiasa huhitajika kuomba Msajili wa Vyama Kisiasa kukisajili.Hakuna chama au shirika ambalo laweza kuendesha shughuli zake kama chama cha kisiasa bila kusajiliwa. Msajili hawezi kusajili chama ama shirika ambalo halijaafiki kanuni ambazo zimeelezewa katika Kifungu cha 91 cha Katiba.

Baada ya kusajiliwa, chama cha kisiasa kinawajibika kukuza umoja wa watu wote, demokrasia na ushiriki wa wananachi katika uundaji wa sera na uteuzi wa wagombea wa uchaguzi.

### Utaratibu wa kusajili vyama vya kisiasa

Usajili wa chama cha kisiasa unafanywa katika viwango viwili; usajili wa muda na usajili kamili.

### Usajili wa muda

Ili kuomba usajili wa muda, chama ama shirika ambalo lina lengo la kuwa chama cha kisiasa lapaswa kutoa ombi kwa ajili ya ukaguzi wa jina la kisiasa kwa Msajili wa Vyama vya Kisiasa. Baada ya jina kuidhinishwa, mwombaji anatoa ombi la usajili wa muda. Jina la chama cha kisiasa hujumuisha jina kamili, ufupisho na nembo.

Msajili anaweza kukataa ombi la usajili wa chama iwapo jina la chama cha kisiasa, ufupisho wa jina ama ishara ambayo chama ina nia ya kutumia ina aibu ama inaudhi,ni jina ama ufupisho ya chama kingine ambacho tayari kimesajiliwa ama kuna ukaribiano wa jina, ufupisho ama ishara na chama kingine ambacho kimesajiliwa ama kitu kingine chochote ambacho kimesajiliwa chini ya sheria nyingine yo yote ambayo imeandikwa.

### Ombi la usajili wa muda

Ombi la usajili wa muda wa chama kinachokusudiwa lapaswa kuwa:

(a) Limeandikwa na kutiwa sahihi na waombaji ambao zaidi ya 2/3 hawatakuwa wa jinsia moja.
(b) Limeambatishwa na kumbukumbu za mkutano wa kwanza wa waanzilishi wa chama cha kisiasa ambazo zimetiwa sahihi.

(c) Limebainisha jina la chama
(d) Iwapo chama kinadhamiria kutumia akronimu ya jina, akronimu ibainishwe
(e) Limeambatanishwa na nakala ya katiba ya chama kinachopendekezwa kwa mujibu wa Sheria (Tazama hapo chini)
(f) Limeambatanishwe na ombi la usajili wa nembo na ishara ya chama.
(g) Limeambatanishwa na ahadi ya kutii Sheria na Kanuni ya Utendakazi
(h) Limeambatanishwa na ada inayohitajika.

Baada ya kupokea ombi la usajili wa muda, Msajili , katika muda wa siku kumi na nne (14) , atatoa tangazo katika Gazeti na magazeti mawili ambayo husambazwa katika nchi nzima na akaribishe pingamizi kutoka kwa mtu ye yote ama chama kingine chochote kuhusu usajili wa jina, nembo na rangi ya chama ama kitu kingine chochote kuhusiana na usajili wa chama hicho.

### Cheti cha usajili wa muda

Baada ya kuthibitisha ukamilifu wa ombi la chama, Msajili atatoa cheti cha usajili wa muda kwa chama kwa kipindi cha siku thelathini (30) baada ya ombi kutolewa.

Chama ambacho kimesajiliwa kwa muda, kwa kipindi kisichozidi siku mia moja na themanini (180) baada ya usajili, kitatoa ombi kwa Msajili kisajiliwe kikamilifu.

Cheti cha usajili wa muda cha chama ambacho kimeomba kusajiliwa kikamilifu kitakuwa halali hadi chama kipate cheti cha usajili kamili ama Ombi Lake, liwe limekataliwa.

## Haki za chama kinachosajiliwa kwa muda .

Chama ambacho kimesajiliwa kwa muda hakina idhini ya kushiriki katika uchaguzi. Chama ambacho kimesajiliwa kwa muda kina idhini ya:-

(a) Kuwa na kuhutubia mikutano ya hadhara katika eneo lolote nchini Kenya kwa lengo la kutangaza chama na kutafuta wanachama.
(b) Kupata ulinzi na msaada kutoka kwa asasi za usalama za nchi kwa lengo la kuwa na mikutano yenye amani na utaratibu na:
(c) Kwa ufadhili wa nchi, kuwa na nafasi ya kutoa mipangilio ya chama kwa umma kupitia vyombo vya habar vya Dola ambavyo vyapaswa kutumikia wote kwa usawa.

Chama ambacho kitakiuka kanuni za usajili wa muda hakitakubaliwa usajili kamili.

## Usajili kamili

Chama ambacho kilikuwa kimesajiliwa kwa muda, kwa kipindi kisichozidi siku mia moja na themanini (180) baada ya usajili, kitahitajika kutoa ombi kwa Msajili kisajiliwa kikamilifu.

Usajili wa muda wa chama ambacho hakitoi ombi la kusajiliwa kikamilifu hufika kikomo baada ya siku 180 kutoka siku kiliyokabidhiwa cheti cha usajili wa muda.

## Ombi la usajili kamili

Ombi la usajili kamili wa chama cha kisiasa lazima litolewe kwa maandishi na liwe limetiwa sahihi na afisa aliyeidhinishwa na chama.

## Masharti ya usajili kamili

Chama cha Kisiasa ambacho kimesajiliwa kwa muda kitakubaliwa usajili kamili baada ya kutimiza marshati yafuatayo:-

(a) Baada ya kupata wanachama wasiopungua elfu moja (1000) waliojisajilisha kama wapiga kura kutoka zaidi ya nusu ya kaunti za Kenya
(b) Wanachama wawe na sura ya maeneo, makabila tofauti, usawa wa kijinsia pamoja na wawakilishi wa makundi maalum.
(c) Viongozi katika chama wawe na sura ya kimaeneo, makabila tofauti, usawa wa kijinsia pamoja na wawakilishi wa makundi maalum.
(d) Viongozi wa chama wasiwe zaidi ya theluthi mbili kwa kila jinsia
(e) Viongozi wa chama wathibitishe kutimiza marshati ya sura ya sita (6) ya Katiba ya Kenya 2010 na sheria zinazohusiana na maadili.
(f) Chama kiwe kimewasilisha kwa Msajili wa Vyama-:

(i) Orodha ya majina, anwani na jinsi ya kutambua wanachama wake wote

(ii) Makao ya ofisi kuu ambayo yamesajiliwa nchini Kenya pamoja na sanduku la posta ambapo matangazo na arifa zingine zinaweza kuwasilishwa
(iii) Makao na anwani za ofisi za matawi ya chama ambazo zinatakiwa kuwepo katika zaidi ya nusu ya kaunti za Kenya.
(iv) Uanishaji wa wanachama kwa misingi ya makundi maalum.

(g) Ahadi ya kutii Sheria na Kanuni za Utendakazi

### Cheti cha usajili kamili

Siku thelathini baada ya kuomba usajili kamilifu na chama kutimiza masharti ya kusajiliwa kikamilifu, Msajili atatoa cheti cha usajili kamili kwa chama cha kisiasa

### Hadhi ya kishirika ya chama kilichosajiliwa kikamilifu

Chama cha kisiasa ambacho kimesajiliwa kikamilifu huwa shirika lenye mkakati wa kujiendeleza pamoja na mhuri na kitakuwa na uwezo kwa mujibu wa jina lake;

(a) Kupata ama kuondoa mali
(b) Kushtaki na kushtakiwa ; na
(c) Kufanya mambo yote ambayo hufanywa na shirika kwa mujibu wa sheria.

## SURA YA NNE: KUFUTA KWA USAJILI WA CHAMA CHA KISIASA

Sheria inampa Msajili nguvu za kufuta usajili wa chama ambacho kimekiuka ama kwenda kinyume na kanuni maalum. Hata hivyo, kabla ya Msajili kufuta usajili wa chama, hatua maalum lazima zifuatwe ili kukipa chama fursa ya kurekebisha makosa yake.

### Sababu za kufuta usajili wa chama

Msajili anaweza kufuta usajili wa chama cha kisiasa iwapo chaa hicho;

(a) Kimejikita katika misingi ya kidini, lugha, rangi, kabila, jinsia ama kieneo ama kinajihusisha na kueneza chuki, ukatili ama kutisha wanachama, wafuasi wapinzani ama mtu mwingine yeyote; ama kina jeshi ama kikundi cha kigaidi ama kinajihusisha na utoaji wa hongo ama aina nyingine ye yote ya ufisadi ama kinatumia mali ya umma kukuza mahitaji yake wakati wa uchaguzi isipokuwa kwa mujibu wa sheria.
(b) Hakizingatii uteuzi wa wagombea kwa uhuru na haki
(c) Hakifuati sheria katika uteuzi wa wagombea
(d) Hakiheshimu maadili ya kitaifa na kanuni za Katiba
(e) Kilipata usajili wake kupitia ufisadi
(f) Kimechangia ama kushiriki katika utendaji wa makosa ya uchaguzi
(g) Kimetenda kinyume na kanuni za kutafuta fedha kwa kutofuata masharti ya fedha za vyama vya kisiasa.
(h) Hakina wawakilishi wa makundi maalumu ;au
(i) Hakidumishi masharti ya usajili kamili

Msajili ana nguvu ya kufuta usajili wa chama kwa misingi ifuatayo:-

(a) Kwa kipindi cha miezi mitatu, chama kinashindwa kutii arifa ya Msajili ambayo inahitaji chama kurekebisha jina lake, Katiba ama sheria
(b) Hakijakuwa na mgombea angalau mmoja wa kiti chochote cha kisiasa kwa vipindi viwili vinavyofuatana vya uchaguzi mkuu na
(c) Kwa kipindi cha siku sitini (60) baada ya kukabidhiwa cheti cha usajili kamili, kinakosa kutoa ama kinatoa stakabadhi bandia juu ya rasilimali na matumizi ya fedha pamoja na michango au misaada ama ahadi za michango ikiwa ya pesa taslimu ama zitatolewa kwa hazina ya awali ya chama na waasisi wake kwa kipindi cha mwaka wa kwanza cha kuwepo kwa chama.
(d) Kwa kipindi cha siku sitini (60) kabla ya uchaguzi mkuu, kinashindwa kutoa ama kinatoa arifa isiyo kweli kwa Msajili kuhusu daftari ya wanachama na arifa juu ya rasilimali zake na madeni kwenye fomu iliyopendekezwa.

Chama cha Kisiasa kinapotenda kosa, Msajili kwa mujibu wa Sheria anaweza;

(a) Kutoa onyo na kutaka chama cha kisiasa kitii Sheria hii kwa kipindi kilichobainishwa.
(b) Kusitisha usajili wa chama cha kisiasa kwa kipindi kisichozidi miezi 12.
(c) Kutotoa fedha kwa chama cha kisiasa kwa kipindi kisichozidi miezi 12 ama
(d) Kwa mujibu wa kipengele cha 21, kufuta usajili wa chama cha Kisiasa.

### Utaratibu wa kufuta usajili wa chama

Kabla ya Msajili kufuta usajili wa chama;

(a) Ataarifu chama kwa maandishi juu ya makosa ama ukiukaji
(b) Ataarifu chama kwa maandishi juu ya nia ya kufuta usajili wake
(c) Elekeza chama jinsi ya kurekebisha makosa ama ukiukaji kwa kipindi cha siku tisini (90) ama kuonyesha sababu kwa nini usajili wa chama hicho usifutwe.

Iwapo chama kitashindwa kurekebisha ama hakishawishi Msajili kuwa makosa hayo hayakutokea kwa kutowajibika ama kutokuwa na nia njema kwa upande wake, kwa kipindi cha siku tisini, Msajili anaweza kufuta usajili wa chama.

Kama usajili wa chama kilichosajiliwa unafutwa, Msajili atatangaza kwa kipindi cha siku kumi na nne (14) notisi ya kufutwa kwa usajili wa chama katika Gazeti la Kenya. Notsi hiyo itatoa siku kamili ya kufutwa kwa usajili.

Iwapo chama cha kisiasa kimetangazwa kama shirika marufuku chini ya sheria nyinginezo, Msajili ana nguvu ya kufuta usajili wa chama hicho.

## Matokeo ya kufutwa kwa usajili wa chama

Msajili atabadilisha hadhi ya chama kutoka kusajiliwa hadi kutosajiliwa katika rejesta ya Vyama vya Kisiasa. Chama kilichopokonywa usajili kitapoteza haki zote za chama cha kisiasa kilichosajiliwa na hasa hakuna mtu ambaye-:

(a) Ataitisha mkutano wa wanachama ama viongozi wa chama isipokuwa kwa lengo la kukomesha shughuli za chama ama kwa lengo la kupinga kufutwa kwa usajili wa chama cha kisiasa;
(b) Atahudhuria ama afanye mtu mwingine kuhudhuria mkutano kama mwanachama ama afisa wa chama hicho cha kisiasa;
(c) Atatoa notisi ama tangazo kuhusu mkutano wa chama hicho isipokuwa kwa lengo lililoelezwa katika (a) hapo juu;
(d) Ataalika watu kusaidia chama hicho.
(e) Atatoa msaada ama mkopo kwa ajili ya michango itakayofanywa kwa manufaa ya chama hicho ama kuipokea michango ama mikopo;
(f) Atatoa dhamana kwa ajili ya fedha kama hizo.

Iwapo chama cha kisiasa kilichofutiliwa usajili kilikuwa na wawakilishi ambao walikuwa wamechaguliwa kama wabunge ama wanachama wa mabunge ya kaunti, wawakilishi hao wataendelea kutumika mpaka mwisho wa kipindi chao kama wawakilishi wa kibinafsi ama wanachama wa vyama vingine vya kisiasa.

Iwapo kufutwa kwa usajili wa chama utatokea kwa makosa ya kimakusudi ama kutowajibika kwa mtu ambaye ni mbunge ama mwanachama wa bunge la kaunti, mtu huyo atapoteza kiti chake cha ubunge ama cha uanachama wa bunge la kaunti.

## Kufunga shughuli za chama cha kisiasa

Baada ya kufutwa kwa usajili wa chama cha kisiasa, Msajili atatangaza kupitia kwa Gazeti la Kenya na kutoa na kumwarifu Mkuu wa Sheria kuhusu kufutw kwa usajili wa chama husika kwa lengo la kutamatisha chama hicho.

## Kusajiliwa tena kwa chama kilichopokonywa usajili

Chama kilichosajiliwa ambacho kimepokonywa usajili chaweza kuamua kuomba kisajiliwe tena. Chama hicho kinaweza kuomba kusajiliwa tena kwa kutoa ombi kwa Msajili kwa kufuata utaratibu unaofuatwa na chama kinachoomba kusajiliwa kwa mara ya kwanza.

### Kufutwa kwa usajili kwa hiari

Chama kilichosajiliwa chaweza kuomba kwa hiari kufuta usajili. Msajili anaweza kukubali ombi hilo la chama kutaka kufuta usajili iwapo ombi hilo limewekwa sahihi na mkuu wa chama na maafisa wengine wawili wa chama.

### Usajili kuahirishwa kwa muda

Msajili anaweza kuweka kando usajili wa chama kwa muda kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na miwili ili kukipatia nafasi ya kurekebisha makosa na kutimiza kanuni za usajili. Chama ambacho usajili wake umewekwa kando kwa muda huwa hakina haki na hakiwezi kufaidika na marupurupu ya vyama vilivyosajiliwa.

### Sababu za usajili kusitishwa kwa muda na matokeo yake

Chama cha kisiasa kinaweza kuwekwa kando kwa muda iwapo hakizingatii kanuni za usajili ama kimefanya makosa kwa mujibuwa Sheria. Lengo la kuwekwa kando ni kupatia chama nafasi ya kurekebisha kosa lililobainishwa katika notisi iliyotolewa na Msajili.

### Matokeo ya kuwekwa kando kwa muda

Iwapo usajili wa chama umekuwa kando ili chama kirekebishe makosa yanayohusiana na kanuni za usajili, chama hicho hakitakuwa na haki zozote na hakiwezi kufaidika na marupurupu ambayo hupewa vyama vilivyosajiliwa kikamilifu kama inavyoelezewa katika Sheria, kipengele cha 15.

## SURA YA TANO: ANAYESTAHILI KUWA MWANACHAMA WA CHAMA CHA KISIASA

Mtu ambaye ni Mkenya na ana umri wa miaka kumi na minane (18) anaweza kuwa mwanachama wa chama cha kisiasa.

### Jinsi ya kuwa mwanachama

Kisheria, Chama cha kisiasa ni chombo ambacho kina haki na majukumu. Kwa hivyo kina uwezo wa kuamua ni nani anaweza kuwa mwanachama na kanuni atakazofuata ili awe mwanachama.

Katiba ya chama huwa na kanuni ambazo huhitaji mtu kutimiza ili awe mwanachama zikiwemo Kanuni za kuwa mwanachama,ada ya kuwa mwanachama,njia za kujiondoa kama mwanachama ,haki na majukumu ya mwanachama wa chama cha kisiasa . Maelezo ya kina yapaswa kuwa kwenye rejesta ya wanachama pamoja na maelezo ya kina juu ya utambulisho; eneo analotoka,

kabila, upungufu, jinsia na kaunti pamoja na utaratibu wa kuendesha mkutano wa mwaka wa chama cha kisiasa.

## Uandikishaji wa wanachama

Uandikishaji wa wanachama utakuwa wa hiari na ni kinyume kuandikisha mtu kama mwanachama wa chama cha kisiasa bila idhini yake.

Kabla chama cha kisiasa kusajiliwa, kinahitajika kutimiza maharti yafuatayo; .

(a) Kuandikisha wapiga kura wasiopungua elfu moja kwa kila kaunti kutoka zaidi ya nusu za kaunti nchini.Wanachama walioandikishwa wapaswa kuwa na sura ya Kenya kwa upande wa maeneo, kabila, usawa wa kijinsia na wawakilishi wa makundi maalum;
(b) Kuhakikisha kuwa watawala wa chama si zaidi ya theluthi mbili kijinsia ;
(c) Orodha ya majina, anwani na njia ya utambulisho ya wanachama iwasilishwe kwa Msajili ; na
(d) Kuhakikisha uainishaji wa data ya wanachama kwa misingi ya makundi maalum.

## Kutokubaliwa kuwa na cheo katika chama cha siasa

Mtu ambaye hakubaliwi kuwa na cheo katika ofisi za umma kwa mujibu wa Katiba na Sheria ama sheria yeyote nyingine ambayo imeandikwa haruhusiwi kuwa na cheo katika uongozi wa chama cha kisiasa ama kuwa mwanachama mwanzilishi wa chama..

## Haki za mwanachama

Mwanachama wa chama cha kisiasa ana haki kadha wa kadha zikiwemo haki za;

(a) Kushiriki katika shughuli za chama ;
(b) Kufanya kampeni za chama ama kusudio lao ;
(c) Kugombea kiti cha uongozi katika chama ;na
(d) Kugombea kiti katika kura ya mchujo ya chama kwa lengo la kuwa mgombea katika uchaguzi mkuu.

### Majukumu ya wanachama wa chama cha kisiasa

Wanachama wa chama cha kisiasa ndio nguzo za chama. Wao ndio hutekeleza majukumu ya msingi ya chama katika jamii yakiwemo:-

(a) Kuhamasisha wananchi kuunga chama mkono;
(b) Kutangamana na kuelimisha wananchi juu ya sera;
(c) Kuandikisha na kuchagua viongozi wa chama;
(d) Kuteua wagombea kutoka kwa chama ambao watashiriki katika uchaguzi mkuu;

(e) Kuunda maoni ya umma kisera;
(f) Kuelimishwa kwa ajili ya uongozi wa siku za usoni ili kudumisha chama;
(g) Kuwakilisha wananchi baada ya kuteuliwa na kuchaguliwa kwenye bunge ama serikali;na
(h) Kulipa ada ya uanachama

### Makundi maalumu

Makundi haya yanajumuisha:-

(a) Wanawake;
(b) Watu wenye ulemavu;
(c) Vijana;
(d) Makabila yenye wananchi wachache; na
(e) Jamii ambazo zimetengwa.

## Vizuizi kwa maafisa wa umma katika chama cha kisiasa

Sheria inaweka vizuizi kwa maafisa wa umma kushiriki katika shughuli za vyama vya kisiasa. Hii inamaanisha afisa wa umma hawezi kuwa mwanzilishi wa chama cha kisiasa,kuwa na cheo cha uongozi katika chama cha kisiasa,kujihusisha na shughuli za chama ambazo huenda zikachukuliwa ama kuonekana kubainisha msimamo wake kuhusiana na ofisi ya afisa huyo ama kuonyesha waziwazi kuunga mkono ama kupinga chama chochote ama mgombea wakati wa uchaguzi.

Kanuni hizi hazihusiki na Rais, Makamu wa Rais, mbunge, gavana, naibu wa gavana ama mbunge wa bunge la kaunti.

## Kutokubaliwa kuwa kiongozi katika chama cha kisiasa

Mtu haruhusiwi kuwa kiongozi katika chama cha kisiasa iwapo si mwananchi wa Kenya, hajaondolewa ufilisi, amehukumiwa kwa makosa ya jinai ambayo yamemfanya kufungwa kipindi kisichopungua miezi sita, ameondolewa kwa kipindi cha miezi sita kwa ajili ya kukiuka kanuni za kimaadili za chama cha kisiasa, haruhusiwi kuwa afisa katika ofisi za umma kwa mujibu wa Katiba, Sheria ya Vyama ama sheria nyingine ye yote ambayo imeandikwa ama amekiuka kanuni za Sura ya Sita ya Katiba ya Kenya 2010.

## Kusitisha kuwa mwanachama wa chama cha kisiasa

Kuna njia nne za mtu kusitisha kuwa mwanachama wa chama cha kisiasa

(a)Kujiuzulu;

(b) Kufukuzwa;
(c)‘Kuonekana;
(d) Kufa

## Kujiuzulu

Mwanachama wa chama cha kisiasa ambaye ana nia ya kujiuzulu anaweza kutoa notisi kabla ya kujiuzulu kwa chama chake, katibu wa kitengo cha bunge kinachohusika ama kwa katibu wa bunge la kaunti iwapo yeye ni mwanachama wa bunge la kaunti. Kujiuzulu huko hutekelewa punde tu notisi yake itakapopokelewa na chama chake,na katibu ambao wote wawili watamjulisha Msajili katika kipindi cha siku saba . Msajili baada ya kupokea notisi hizo, atafuta jina la wanachama huyo kutoka rejesta ya wanachama wa chama cha kisiasa kinachohusika.

## Kufukuzwa

Mwanachama wa chama cha kisiasa anaweza kukoma kuwa mwanachama kwa kufukuzwa kutoka kwa chama .Katiba ya chama huwa na mikakati ya kudhibiti wanachama wake.Mwanachama anaweza tu kufukuzwa iwapo ametenda kinyume na masharti ya Katiba ya Chama na baada ya kupewa fursa ya kujitetea kwa mujibu wa sheria za ndani za kusuluhisha mizozo kama inavyoelezewa kwenye Katiba ya Chama. Katiba ya chama lazima iwe na utaratibu wa kuhimiza nidhamu ambao umejikita katika vitendo vyenye haki vya kiutawala kama inavyobainishwa kwenye Kifungu cha 47 cha Katiba

## ‘Kuonekana’

Njia nyingine ya mtu kukoma kuwa mwanachama wa chama cha kisiasa ni kutokana na “kuonekana “kama amejiuzulu, Mwanachama wa chama cha kisiasa anaweza kuonekana kama amejiuzulu kutoka kwa chama hicho iwapo:

(a) Ameunda chama kingine cha kisiasa;

(b) Anahusika katika uundaji wa chama kingine cha kisiasa;

(c) Anajiunga na chama kingine cha kisiasa

(d) Kwa njia ye yote ile, anapendekeza uundaji wa chama kingine cha kisiasa;

(a)/Anakuza itikadi, maazimio ama sera za chama kingine cha kisiasa.

Chama cha kisiasa ambacho mwanachama wake ameonekana kama amejiuzulu kwa mujibu wa utaratibu uliotolewa katika Katiba ya chama husika, kitajulisha Msajili kuhusu uamuzi huo kwa kipindi cha siku saba.

## SURA YA SITA: KATIBA AMA KANUNI ZA CHAMA CHA KISIASA

Sheria inahitaji katiba ama kanuni za chama kutoa mwongozo juu ya mambo yaliyobainishwa hapa chini. Zaidi ya hayo, katiba ama sheria za kila chama cha kisiasa lazima zihakikishe kwamba wanachama wake hawazidi theluthi mbili kwa kila jinsia katika vitengo vyote vya chama pamoja na kamati.

Pale ambapo chama hakitimizi kifungu chochote cha Sheria, Msajili anaweza kujulisha chama kwa maandishi na ahimize chama kurekebisha katiba ama kanuni zake katika kipindi cha miezi mitatu na iwapo chama hakitatekeleza matakwa hayo, usajili wake utafutwa.

### Mambo ambayo yapaswa kuzingatiwa katika katiba ama kanuni za chama

Katiba ama kanuni za chama chochote lazima zizingatie mambo yafuatayo:-

(a) Jina la chama cha kisiasa na ufupisho wake iwapo upo;
(b) Nembo ama ishara ya chama cha kisiasa na rangi zake;
(c) Malengo ya chama cha kisiasa;
(d) Ieleze kinagaubaga maono, mwelekeo, maadili na kanuni zinazoongoza chama
(e) Makao na Sanduku la posta na ofisi ya chama kilichosajiliwa
(f) Kanuni za uanachama zikiwa ni pamoja na:-

(i)Kigezo cha mwanachama;

(ii)Ada ya mtu anapojiunga na chama na malipo ya uanachama;

(iii)Kigezo cha mtu kujizulu kutoka kwa chama ama kuacha kuwa mwanachama;

(iv)Haki na majukumu ya wanachama;

(v)Maelezo ya kina juu ya wanachama pamoja na maelezo ya kina juu ya utambulisho, eneo, kabila, ulemavu, uana na kaunti;

(vi)Utaratibu wa kuendesha mkutano wa mwaka ama mkutano mwingine wo wote wa chama pamoja na mambo ambayo yanaweza kuamuliwa tu katika mkutano wa wanachama ama wawakilishi wa bunge la kaunti kama inavyostahili.;na

(vii)Hitaji la kuboresha rejesta ya wanachama kila mara.

(g) Mahitaji ya kundi litakaloongoza ni:-

(i) Jina la kundi linaloongoza ;
(ii) Kigezo cha kuchaguliwa katika kikundi cha kuongoza;
(iii) Cheo, jina na muda wa kuwa katika ofisi;
(iv) Haki na majukumu ya mwanachama katika kikundi cha uongozi;
(v) Utaratibu wa kuchagua wanachama wa kikundi cha uongozi na vitengo vingine vya chama ikiwa ni pamoja na kamati;
(vi) Miongozo ya utendakazi wa kikundi cha uongozi na kamati zake;
(vii) Idadi ya wanachama wanaohitaji kuwepo ili mkutano uendelee (akidi)
(viii) Idadi ya mikutano itakayofanyika; na
(ix) Nguvu za kutoa maamuzi
(x) Miongozo ya mikutano, utaratibu wa kuitisha mikutano, utaratibu wa kuendesha mikutano na njia rasmi ya kuandika maazimio ya mikutano.

(h) Orodha ya vitengo vya utawala na mifumo iwe Imeandikwa katika afisi za chama cha kisiasa pamoja na:-

i. Maelezo kamili ya wafanyikazi na masharti ya uajiri wao;
ii. Sera taratibu za rasilimali watu;
iii. Matawi madogo ya chama katika kila kaunti.

(i) Uundaji wa matawi ya chama yakiwemo matawi yale ya nje ya; nchi pamoja na wajibu na majukumu yao.
(j) Muundo na mfumo wa kifedha pamoja na:

(i) Wajibu na majukumu ya maafisa binafsi, vitengo na vyombo vya utawala kuhusiana na masuala ya fedha katika chama cha kisiasa.

(ii) Tathmini ya kisheria ya matumizi ya fedha za chama ya kila mwaka; na

(iii) Mambo ambayo yanaweza kufanya pesa zitumike na hasa vikwazo vya wanachama kugawiwa pesa.

(k) Muundo wa kijumla na usimamizi wa chamacha kisiasa pamoja na miundo na taratibu na vitengo vya uongozi katika kaunti
(l) Uundaji na usimamizi wa makundi ya Bunge la kitaifa, Seneti na mabunge ya kaunti.
(m) Mikakati ya kuadhibu mwanachama ama afisa wa chama ikiwemo:

(i) Mbinu na utaratibu wa kutoa adhabu kwa mujibu wa Vifungu 47 na 50 vya Katiba.

(ii) Vitendo vinavyoweza kutumika kumwadhibu mtu na sababu zake;

(iii) Vigezo vya vitendo mbalimbali vya nidhamu;

(iv) Matokeo ya kila kitendo katika kiwango cha kitaifa na cha kaunti;

(n) Haki ya kukagua vitabu za orodha ya wanachama na mwanachama wa chama ama mwananchi;

(o) Afisa wa chama walioidhinishwa wataweka sahihi kwa niaba ya chama;

(i) Stakabadhi zote zitakazowasilishwa kwa Msajili zikiwemo rejesta ya wanachama, miseto na ripoti zingine;
(ii) Hesabu na namba za akaunti za benki za chama;
(iii) Tahmini za mwaka za matumizi ya fedha za chama pamoja na maelezo ya fedha ya chama;
(iv) Ripoti yo yote ama stakabadhi ya chama ambayo inahitajika kisheria ama kwa mujibu wa sheria yo yote iliyoandikwa; na
(v) Vyeti vya uteuzi kwa uteuzi wo wote ama uchaguzi wa mwanachama wa chama cha kisiasa;

(p) Stakabadhi za sera ambazo chama kitatunga ili ziwe mwongozo wa utendakzi ikiwemo njia na taratibu ambazo zitatumika kuzitunga, kuziidhinisha na kuzitekeleza.

(q) Stakabadhi za kutoa ripoti za sera na wakati wake wa kuzitoa ikiwemo njia na taratibu zitakazotumika kuzitunga kuziidhinisha na kuzitangaza;

(r) Sera na taratibu za kudhibiti rasilimali, uhifadhi wa fedha na mali za chama na uteuzi wa watu watakaozisimamia

(s) Kanuni na taratibu za chama cha kisiasa juu ya:

(i) uchaguzi wa maafisa wa chama;

(ii) Uteuzi wa wagombea wa uchaguzi;

(iii) Uteuzi wa wagombea watakaowekwa kwenye orodha ya chama.

(t) Mahitaji ya kubadilisha jina, ishara, rangi za chama, Katiba na kanuni za chama.

(u) Kanuni za miseto ikiwa ni pamoja na:

(i) Muktadha na vigezo vya miseto na;

(ii) Kanuni na miongozo ya miseto kama hiyo kama inavyoidhinishwa na mkutano wa chama wa mwaka.

(e)Kanuni za kujiunga na miseto.

(w) Masharti ya kuvunja chama yakiwemo:

(i) Masharti ya jinsi kutoa mali ya chama; na

(ii) Jinsi na kanuni za kufuata wakati wa kuvunja chama ama tawi lolote la chama

(x)Suluhu ya migogoro ya ndani ya chama kwa mujibu wa Kifungu cha 47 na 50 cha Katiba.

(y) Utendaji wa kidemokrasia ambao unazingatia jinsia, tendosawazishi kwa ajili ya makundi ya walio wachache na waliotengwa.

(z) Onyesha utendaji wa kidemokrasia ambao unazingatia haki za kibinadamu na kijinsia.

(a) Mbinu za kutekeleza maadili ya kitaifa na kanuni za uongozi kwa mujibu wa Katiba.

## SURA YA SABA: MIUNGANO NA MISETO

### Miungano

Muungano ni uimarishaji au mchanganyiko katika chama cha kisiasa au kuunganisha vyama viwili au zaidi vya kisiasa ili kuunda chama kimoja.. Muungano huu unaweza kutokea wakati wowote isipokuwa kipindi chochote kinachoanzia siku thelathini (30) kabla ya kutoa hati kwa ajili ya uchaguzi na kumalizika siku ya uchaguzi.

### Malengo ya vyama ya kuungana.

Vyama vya kisiasa vinaweza kuungana ili:-

(a)Kupata kura zaidi wakati wa uchaguzi;

((b)Kupata vyeo zaidi vya mawaziri;

(c)Kubadilisha sura ya chama cha kisiasa.

(d) kutia nguvu ajenda ya sera kupatia chama chenye nguvu zaidi na kikubwa zaidi;

(e)Kuwakilisha na kuvutia wanachama wengi zaidi kupitia kwa chama kikubwa zaidi;

(f)Kuchanga pesa zaidi kutoka kwa umma na watu binafsi na kuepuka kutumia fedha kushindana wenyewe kwa wenyewe; na

(g)Kuhakikisha chama cha tatu kisichotakikana hakitakuwa kwenye serikali.

## Utaratibu wa kuomba muungano

Ili chama cha kisiasa kiungana na chama kingine cha kisiasa, sharti kitimize mahitaji ya Katiba, Sheria ya Vyama vya Kisiasa na Kanuni na Utaratibu wa vyama vya Kisiasa. Uamuzi wa kuungana lazima ufanywe kwa maandishi na utekelezwe na maafisa walioruhusiwa kutekeleza mikataba kwa niaba ya vyama vya kisiasa.

Chombo tawala cha kila chama cha kisiasa ambacho kina nia ya kuungana kitabainisha katiba, sheria na kanuni na mihimili ambayo itakuwa msingi wa muungano kwa mujibu wa katiba za vyama vya kisiasa vinavohusika na kuweka sahihi mkataba wa muungano.Mkataba wa muungano uliotiwa sahihi utawasilishwa kwa Msajili wa vyama katika kipindi cha siku ishirini na moja (21) baada ya kutiwa sahihi.

Baada ya kupata chombo cha muungano, Msajili anahitajika mara moja kufuta vyeti vya usajili vya vyama vyote vya kisiasa ambavyo vimeungana na atatangaza kuvunjwa kwa vyama hivyo katika kipindi cha siku saba na kutoa cheti cha usajili kamili kwa vyama vilivyoungana katika hicho chama kipya cha kisiasa.

## Uanachama wa chama cha muungano

Iwapo chama kimeungana, mwanachama wa chama cha kisiasa kilichoungana atachukuliwa kuwa mwanachama wa chama kipya cha kisiasa.

Mwanachama ambaye ni Rais, Makamu wa Rais, Gavana na makamu wa Gavana, mbunge ama mwanachama wa Bunge la kaunti na ambaye hapendi kuwa mwanachama wa chama kipya cha kiasa ambacho kimesajiliwa baada ya muungano, ataendelea kuhudumu katika kitengo chake kwa kipindi kilichosalia ama ajiunge na chama kingine ama achague kuwa mwanachama wa kibinafsi kwa kipindi cha siku thelathini (30) baada ya chama kipya kusajiliwa.

## Athari za muungano

Iwapo vyama vya siasa vimeungana na vile vya awali vimevunjwa, utambulisho wao ikiwa ni pamoja na majina, ishara, nembo na rangi zao zitaondolewa kutoka kwa rejista ya Msajili wa vyama na majina, ishara, nembo na rangi hizo hazitatumika kusajili chama kipya cha kisiasa kwa uchaguzi utakaofuatia baada ya muungano.

Iwapo vyama vilivyoungana vitapendelea kusajili na kutumia majina, ishara, nembo, wito ama rangi za chama cha awali, wataruhusiwa kufanya hivyo. Hazina ya Vyama vya Kisiasa, madeni, haki na wajibu wa vyama vyote vilivyovunjwa, vitakuwa ndivyo kumbukumbu, vito vya thamani, madeni, haki na wajibu wa chama kipya ikiwemo haki ya kupata fedha kutoka Hazina ya Vyama vya Kisiasa.

## Mseto

Mseto ni muungano wa vyama viwili au zaidi vya kisiasa ambavyo vinaundwa kwa lengo la kufikia azimio la pamoja na ambao unatawaliwa na mkataba ambao umeandikwa na kuwasilishwa kuwa Msajili. Mseto huwezesha vyama husika kufuatilia maazimio ya pamoja. Mseto ni tofauti na miungano kwa vile vyama mbali na kushirikiana vinabakia na utambulisho wa kisheria na huwa na viongozi, katiba, wanachama wake na kadhalika.

Vyama vya kisiasa vyaweza kutia sahihi mkataba wa kushirikiana kabla ya uchaguzi (mseto wa kabla ya uchaguzi) ama baada ya uchaguzi (mseto wa baada ya uchaguzi).

Malengo ya miseto ni kuwa na miungano ambayo itawasaidia kutimiza malengo ya pamoja kama vile kushinda katika uchaguzi na kuunda serikali ama kuimarisha jukumu lao kama wapinzani.

### Mikataba ya mseto

Sheria ya Vyama vya Kisiasa inaruhusu vyama viwili au zaidi kuungana pamoja kuunda mseto kabla ama baada ya uchaguzi kwa kuwasilisha mkataba wa makubaliano kwa Msajili.

Mkataba wa mseto wapaswa kuzingatia kanuni na taratibu za vyama vya kisiasa kuhusu uundaji wa mseto.

Mseto huu lazima uidhinishwe na chombo tawala cha vyama vya kisiasa ambavyo vinahusika katika mseto na sharti:

uwe katika hali ya maandishi na utekelezwe na maafisa wa kitaifa wa vyama vya kisiasa na

(a)Uwe umepitishwa na hakimu wa viapo.

## Mkataba wa mseto lazima ueleze-:

(a) Vyama ambavyo ni wanachama wa mseto;
(b) Sera na malengo ya mseto;

(c) Muundo wa mseto;
(d) Muundo wa kijumla na uongozi wa mseto, pamoja na miundo na mifumo ya kaunti na vitengo tawala katika kaunti.
(e) Mbinu na vigezo vya kugawanya nafasi katika muundo wa mseto, wajibu na majukumu katika mseto;
(f) Sheria za uchaguzi katika mseto;
(g) Sheria za uteuzi kwenye mseto
(h) Kitengo cha uamuzi, kanuni na utaratibu;
(i) Mchakato na taratibu ambazo zitaongozwa kubadilishwa kwa makubaliano ya mseto ikihitajika;wa kuanzisha sera, kushauriana juu ya sera, sharia na utaratibu.
(j) Muundo, kanuni na taratibu za kuanzisha sera, kushauriana juu ya sera na kufanya maamuzi kuhusu sera;i za utendakazi kwenye mseto pamoja na maadili na mihimili ya kuongoza utendakazi wa watu binafsi na wanachama kwenye mseto.
(k) Kanuni za Maadili za mseto ikiwa ni pamoja na maadili na kanuni zinazoongoza utendaji wa watu binafsi na vyama wanachama vya mseto;
(l) Mbinu na taratibu za kusuluhisha migogoro kwenye mseto;
(m) Mbinu za kutekeleza adhabu na taratibu za kuadhibu wale wanaoenda kinyume na makubaliano ya mseto;
(n) Utaratibu wa kupata nafasi ya kupeleka malalamiko kwa mahakama;
(o) Jukumu la chombo tawala na vitengo vya vyama vya kisiasa vya vyama binafsi vya katika mseto kuhusu uendeshaji wa shughuli za mseto ikiwemo uhusiano, utaratibu na kanuni lengwa.
(p) Vigezo na utaratibu wa kugawanya pesa kutoka Hazina ya Vyama vya Kisiasa kwa kila chama kwenye mseto; na
(q) Sababu ambazo zaweza kuchangia kuvunjwa kwa mseto zikiwemo taratibu na kanuni ambazo zitafuatwa.

## Aina za miseto

Sheria inaruhusu vyama vya siasa kuunda miseto kabla na baada ya Uchaguzi

## Mseto wa kabla ya uchaguzi

Huu ni mkataba wa mseto ambao unaundwa kabla ya uchaguzi. Mkataba wa mseto lazima uwasilishwe kwa msajili miezi tatu kabla ya Uchaguzi. Katika mkataba huu wa kabla ya uchaguzi vyama vya mseto hukubaliana kuwa wana nia ya kuunda serikali wakiwa pamoja iwapo watapata kura za kutosha katika uchaguzi utakaofanyika karibuni.

Mseto wa kabla ya uchaguzi waweza kuwa wa ushirikiano huru ama thabiti na waweza kuwa-:

(a) Tangazo tu kuwa watafanya kazi pamoja;

(b) Uhusiano huru kama kuhimiza wapiga kura kumpigia kura mshirika wao

(c) Tangazo la kuwa na jukumu la sera ya pamoja;

(d) Majadiliano juu ya jinsi ya kujiondoa Hii inamaanisha kuwa:mgombea wa chama kimoja katika eneo la uchaguzi fulani na mgombea wa chama kingine katika eneo lingine la uchaguzi hivi kwamba washiriki hao wawili hawashindani katika eneo lolote la uchaguzi.wakatika wa uchaguzi katika maeneo ya uchaguzi.

## Mseto wa baada ya uchaguzi

Huu ni mkataba wa mseto ambao unaundwa baada ya uchaguzi. Lazima mkataba huu wa mseto uwasilishwe kwa Msajili katika kipindi cha siku ishirini na moja (21) baada ya kuwekwa sahihi. Miseto ya baada ya uchaguzi mara nyingi huwa ni miseto ya serikali ambayo huamua:

(a)Nini atahusishwa kama mwenza katika serikali na vigezo vya uhusiano;
(b) Sera za pamoja ambazo serikali itatekeleza.

Mara nyingi vyama hukubaliana juu ya haya kwa msaada wa mkataba wa mseto.

Makubaliano ya mseto hujikita katika mambo kama jinsi ya kugawanya vyeo, uundaji wa serikali, sheria za kuamua mambo katika mseto, utaratibu wa kuamua mambo kwa pamoja, mpango wa serikali kuhusu sera ushirikiano katika uchaguzi na kuachishwa kazi kwa mawaziri na kipindi cha kutumika.

## Matokeo ya kuunda mseto

Kila chama kwenye mseto hubaki na utambulisho wake kisheria na huwa huru kisheria kutoka kwa vyama vingine katika mseto. Chama hicho huwa na haki zake na majukumu yake pamoja na madeni yake kwa mujibu wa sheria ya vyama na sheria zingine.

Mseto:

(a)Hauna haja ya kusajili jina la mseto lakini unaweza kutumia jina lo lote kuufanya mseto uwe na umaarufu;
(b) Hauna haja ya kusajili wito wake, nembo ama rangi lakini unaweza kuzitumia kuupa umaarufu.

(c) Unaweza kutumia nembo, ishara na rangi za vyama ambavyo vimeshirikishwa kwenye mseto;
(d) Haupati fedha kutoka kwa hazina ya fedha vya vyama lakini vyama vyenyewe hupata
(e) Huweza tu kukubali vyama vya kisiasa vilivyosajiliwa kama wanachama wake;
(f) Hauna haja ya watu binafsi kuwa wanachama isipokuwa kupitia kwa vyama vinavyohusishwa kwenye mseto; na
(g) Hakuna mgombea atakayeteuliwa kwa tikiti ya mseto.

### Kubadilisha mkataba wa mseto

Mkataba wa mseto unaweza kubadilishwa lakini lazima ufuate kanuni za Sheria za Vyama vya Kisiasa mkataba wa mseto na kanuni zilizoelezwa wazi katika mkataba wa mseto wa kwanza.

### Kuvunja mseto

Mseto unaweza kutamatishwa kwa kufuata sheria zilizoelezwa wazi katika mkataba wa mseto.

## SURA YA 8: MFUMO WA USIMAMIZI WA VYAMA VYA KISIASA

### Rekodi za chama cha kisiasa

Stakabadhi za chama ni muhimu katika kukifanya chama kuwa taasisi, kushiriki kwa wanachama, mafunzo kwa wanachama na umma kwa jumla, uwajibikaji, uwazi na uwakilishaji ufaao. Kwa hivyo, vyama vyote vya kisiasa sharti viwe na stakabadhi zifuatazo zilizo sahihi na za kuaminika:

(a) katiba au kanuni za chama cha kisiasa;

(b) kanuni za chama kuhusu uchaguzi;

(c) kanuni na mwongozo wa chama kuhusu uteuzi wa mchujo;

(d) kanuni za maadili za vyama vya kisiasa;

(a) Sajili iliyokamilika ya wanachama katika afisi kuu;

(b) majina na habari za mawasiliano ya maafisa wa chama na viongozi waliochaguliwa;

(c) bajeti ya chama, habari za mchango ikiwa ni pamoja na malipo ya ada ya uanachama, ripoti za ukaguzi wa fedha zilizofanywa siku za karibuni pamoja na taarifa kuhusu mali ya chama.

(d) stakabadhi zinzohitahijika wakati wa kipindi cha uchaguzi ikiwa ni pamoja na orodha ya wagombeaji katika chama, wanachama walioteuliwa pamoja na orodha ya wanachama (wakati wa uchaguzi);

(e) stakabadhi nyinginezo zenye mpango wa chama pamoja na mpango mkakati, manifesto nk.

## Afisi ya kaunti

Ili chama kiweze kusajiliwa, kinahitajika kufungua afisi za chama katika angalau nusu ya kaunti zote nchini Kenya. La umuhimu zaidi ni kuwa sharti afisi hizo ziwe zinafanya kazi. Afisi za vyama za kaunti ni muhimu katika kutoa huduma kwa chama na kwa umma kwa ujumla.

Chama cha kisiasa kinahitajika kuweka katika afisi zake za kitaifa na zile za kaunti, rekodi halisi za:

(a) sajili ya wanachama waliojiandikisha kwenye fomu iliyoagizwa;

(b) nakala ya Katiba ya chama hicho;

(c) nakala ya sera na mipango ya chama hicho cha kisiasa;

(d) habari za mchango au msaada au ahadi ambayo imetolewa na waanzilishi wa chama hicho cha kisiasa ikiwa pesa taslimu au bidhaa;

(e) makadirio ya matumizi ya fedha za chama kulinga na sheria inayohusu usimamizi wa fedha za umma;

(f) habari za mali yoyote inayomilikiwa na chama na wakati pamoja na namna mali hiyo ilivyopatikana;

(g) vitabu vya chama vinavyohusu matumizi ya fedha ambavyo vimekaguliwa siku chache zilizopita kwa mujibu wa kanuni za ukaguzi wa fedha za umma kulingana na sheria hii vikionyesha:

(i) Mahali ambapo fedha hizo zilitoka, majina, habari za mawasiliano pamoja na habari nyinginezo muhimu ambazo Msajili wa vyama anaweza kuulizia;

(ii) Ada ya uanchama ambayo imelipwa;

(iii) Msaada ukiwa pesa taslimu au kwa njia nyingineyo;

(iv) Mchango usio wa moja kwa moja kwa chama na risiti zote za mchango huo ikiwa ni pamoja na fedha zinazopokelewa na zile zilizotumiwa kwa shughuli za chama;

(v) Kila shughuli ya fedha na rekodi za raslimali na madeni ya vyama; na

(vi) habari zingine muhimu kama atakavyohitaji Msajili.

Mwanachama wa chama cha kisiasa anaweza wakati wowote wa kazi na badala ya kulipa ada zilizoamriwa akahitaji kuchunguza na kutaka apewe nakala za chama cha kisiasa ambazo ziko kwenye afisi za kaunti au za kitaifa. Mtu yeyote anaharibu au kutekeleza rekodi za chama cha kisiasa ambacho kimesajiliwa huwa amevunja sheria.

Kulingana na Sheria ya Vyama vya Kisiasa, mahitaji ya chini zaidi ni kuwa sharti afisi za vyama vya kisiasa ziwe zinafanya kazi, zinaweka rekodi ambazo zinaweza kutolewa kwa wanachama na umma kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kutoa nakala za rekodi hizo ikiwa watahitaji.

### Ukaguzi wa rekodi za vyama vya kisiasa

Msajili anaweza kutoa notisi kwa njia ya maandishi, kwa Mwenyekiti au Katibu Mkuu wa chama cha kisiasa akitaka apewe kwa ajili ya ukaguzi stakabadhi zinazohitajika kuwepo katika afisi za chama au habari nyinginezo ambazo zinaweza kupatikana ili kutimiza yaliyomo kwenye sheria. Msajili anaweza kutolesha nakala za au kuchukua sehemu au dondoo kutoka kwenye rekodi za chama akilenga kupata habari zozote kulingana na sheria hizi.

Mwenyekiti au Katibu Mkuu wa chama cha kisiasa sharti aheshimu notisi iliyotolewa na Msajili kulingana na sehemu ya (1). Mwenyekiti au Katibu Mkuu wa chama cha kisiasa atakuwa amevunja Sheria ikiwa atakosa kufuata maagizo ya notisi ya msajili kama ilivyo katika sheria hii.

### Mikutano ya umma ya chama cha kisiasa

Chama cha kisiasa ambacho kimesajiliwa kikamilifu kinahitajika kufanya mikutano ya chama katika viwango vya kitaifa na katika kaunti kwa mujibu wa katiba ya chama. Chama cha kisiasa kinachotarajia kuandaa mkutano wa hadhara kitahakikisha kuwa kinazingatia yaliyomo kwenye sheria inayohusu maandalizi ya mikutano ya hadhara.

## SURA YA 9: UTAWALA WA FEDHA

Sheria hii inatoa mwongozo mzuri kuhusu ufadhili wa vyama vya kisiasa na namna uhasibu unavyofanywa. Sababu ya kufanya hivi ni kuhakikisha kuwa kuna matumizi mazuri ya fedha hizo. Hazina ya Vyama vya Kisiasa husaidia kuleta uwajibikaji, uwazi pamoja na ushindani wa

kisawasawa baina ya vyama. Hili kimsingi linasaidia kukabiliana na ufisadi kwa kuzingatia haki za wahusika kama ilivyo kwenye katiba.

Sheria hii pia inatoa mwongozo wa ugavi au kugawanywa kwa fedha za hazina hiyo, inadhibiti wafadhili wa vyama, inaeleza mahali ambapo fedha hizo zinatoka mbali na kutoa maelezo ya namna fedha hizo zilitumika. Sababu za kwa nini fedha hizo zinafaa kugawanywa zimefafanuliwa katika sheria hii na zinazingatia demokrasia.

## Mahali ambapo fedha za vyama vya kisiasa hutoka

Fedha za vyama vya kisiasa kwa:

(a) hazina ya Vyama vya Kisiasa;
(b) ada ya uanachama;
(c) mchango kutoka kwa wafadhili kwa kutumia njia zifaazo kisheria;

(d) michango, urithi na ufadhili kutoka kwa watu au makundi yanayokubalika kisheria, na ambao si wageni au serikali za kigeni au shirika lisilo la kiserikali; na

(e) faida inayotokana na uwekezaji, mradi au shughuli yoyote ya chama cha kisiasa.

## Hazina ya Vyama vya Kisiasa

Sheria hii imeruhusu kuwepo kwa hazina ijulikanayo kama Hazina ya Vyama vya Kisiasa, ambayo husimamiwa na msajili wa vyama vya kisiasa. Serikali hutoa fedha za Hazina ya Vyama vya Kisiasa ili zitumike katika kufadhili shughuli mbalimbali za vyama ambazo zinaambatana na mwongozo ambao umetolewa katika sheria hii.

### Chanzo na sababu za kuwepo kwa hazina ya vyama vya kisiasa

Vyama vya kisiasa huhitaji fedha ili kushughulikia masuala ya kimsingi yanayohusu chama. Awali ya yote, fedha za vyama zinatokana na michango ya wanachama, mchango kutoka kwa wafadhili, pamoja na harambee au shughuli za kuchangisha fedha. Vyanzo hivi vya fedha vinaonyesha kuwa vyama vya kisiasa vimejengwa kutokana na jamii na hivyo vinahusisha wanachama wake kikamilifu badala ya kutegemea ufadhili wa serikali pekee.

Sheria ya Vyama vya Kisiasa ya mwaka wa 2007 iliidhinisha kuwepo kwa Hazina ya Vyama vya Kisiasa ambayo inafadhiliwa na serikali na kusimamiwa na Msajili. Hazina hiyo bado imesalia katika Sheria ya Vyama vya Kisiasa ya mwaka wa 2011.

Lengo la hazina hii ni kusaidia vyama vya kisiasa kutimiza majukumu yake katika jamii ya kidemokrasia hasa wakati ambao si wa uchaguzi.

## Malengo ya hazina

Vyama vya kisiasa vinatakiwa kutumia fedha kutoka kwa Hazina hii kwa njia zifuatazo:

(a) angalau asilimia thelathini (30%) ya fedha za Hazina hiyo zinafaa kufanikisha uwakilishi wa akina mama, watu wanaoishi na ulemavu, vijana, kabila ndogo na jamii zilizotengwa katika bunge la kitaifa na la kaunti;

(b) kuhakikisha kuwa mwananchi wanahusishwa katika siasa za nchi;

(c) kushughulikia gharama za uchaguzi mbali na kutangaza sera za chama cha kisiasa katika vyombo vya habari;

(d) katika kusaidia chama cha kisaisa kuandaa mafunzo ya uraia kuhusu demokrasia na shughuli za uchaguzi;

(e) kukisaidia chama cha kisiasa kujiuza kwa umma; na

(f) angalau asilimia thelathini (30%) ya fedha hizo (hicho kikiwa kiwango cha juu za fedha) zitumike katika kugharimia shughuli za utawala na malipo ya wafanyakazi.

## Mahali fedha za hazina hii zinatoka

Fedha za hazina hii hutoka kwa;-

(a) ushuru ambao sio chini ya asilimia 0.3 ya fedha zote zinazokusanywa katika ushuru wa serikali kuu kama inakavyoidhinishwa na bunge; na

(b) mchango kutoka kwa watu au makundi yoyote yanayoruhusiwa kisheria.

Mahali kwingine ambako fedha za vyama vya kisiasa hutoka ni:

(a) Ada za uanachama;

(b) mchango kutoka kwa wafadhili kwa kutumia njia zifaazo kisheria;

(c) misaada, urithi au ufadhili kutoka kwa watu au makundi yanayokubalika kisheria, na ambao si wageni au serikali za kigeni au shirika lisilo la kiserikali; na

(d) faida inayotokana na uwekezaji, mradi au shughuli yoyote ya chama cha kisiasa.

Baada ya mwaka wa kifedha kukamilika, masalio yoyote ya fedha za vyama vya kisiasa itawekwa ili kufadhili shughuli ambazo zimetengwa kisheria kwa kuzingatia sheria yoyote kuhusu matumizi ya fedha za umma.
Chama cha kisiasa kitaweka wazi kwa Msajili ripoti ya fedha na raslimali zote za chama na mahali zilikotoka.

Chama cha kisiasa kinatakiwa katika muda wa siku tisini baada ya kukamilika kwa mwaka wa matumzi ya fedha, kuchapisha;

(a) mahali ambapo fedha za chama zilitoka kwa kufafanua;

  (i) kiwango cha fedha zote zilizopokelewa kutoka kwa Hazina;

  (ii) kiwango cha fedha zote zilizopokelewa kutoka kwa wanachama na wafuasi wa chama; na

  (iii)kiwango cha fedha zote zilizotokana na mchango pamoja na waliochanga;

(b) fedha zilizopokelewa na zilizotumiwa na chama; na

(c) rasilimali na madeni ya chama.

Chapisho hilo linafaa kuwekwa katika angalau magazeti mawili makuu yanayofika pembe zote za taifa. Chama chochote cha kisiasa ambacho kitavunja sheria hii kitazuiliwa kupokea fedha kutoka kwa Hazina hiyo kwa kipindi hicho ambacho hakitakuwa kimetimiza kifungu hiki cha sheria.

## Vizuizi vya kutumia fedha za Hazina

Vyama vya kisiasa vinazuiliwa kutumia fedha kutoka kwa Hazina hiyo ili:

(a) kuwalipa wanachama au wafuasi wasiokuwa wafanyakazi wa chama mshahara, ada, tuzo marupurupu au malipo ya aina yoyote kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja;

(b) kugharimia au kutoa mchango wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja kwa jambo, tukio au shughuli yoyote kinyume na kanuni ya maadili ya wafanyakazi wa umma;

(c) kuanzisha kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja biashara au kujitengenezea faida kutokana na mali yoyote itokanayo na fedha za hazina; au

(d) kutumia fedha hizo kwa njia yoyote ambayo haiambatani na haiendelezi demokrasia ya vyama vingi na shughuli za uchaguzi au Katiba.

Vyama vya kisiasa vinatakiwa kuhakikisha kuwa kuna uwajibikaji na uwazi katika shughuli ya kununua bidhaa. Sheria inasema kuwa ni hatia kwa chama cha kisiasa kutumia fedha katika zake kwa njia nyinginezo mbali na zile zilizopo kwenye sheria.

## Masharti ya kutimiza ili kupata mgao wa fedha za hazina ya vyama vya kisiasa

Si vyama vyote vilivyosajiliwa vinaweza kupokea mgao wa fedha kutoka kwa Hazina ya Vyama vya Kisiasa.Lazima chama cha kisiasa kitimize masharti yafuatayo ili kupata mgao huo:

(a) Kipate angalau asilimia tano ya idadi ya kura zilizopigwa wakati wa uchaguzi mkuu uliopita;
(b) Kifanikishe usawa wa jinsia ili kuhakikisha kuwa hakuna jinsia inayowakilishwa na zaidi ya theluthi mbili ya watu wa jinsia moja.

Pia, chama cha kisiasa hakiwezi kupokea mgao wa fedha za Hazina ya Vyama vya Kisiasa ikiwa:

(a) Chama hakikupata angalau asilimia tatu ya kura zote zilizopigwa katika uchaguzi uliotangalia;

(b) Ikiwa theluthi mbili ya viongozi wa wanachama waliosajiliwa ni ya aina moja ya jinsia;

(c) Chama hakina wawakilishi wa makundi maalum katika uongozi wake; au

(d) Chama hakina angalau:

(i) Wabunge 20 waliochaguliwa katika bunge la kitaifa;

(ii) Wabunge watatu wa bunge la Seneti;

(iii) Wanachama watatu ambao ni magavana; na

(iv) Wabunge 45 wa mabunge ya kaunti.

## Ugawaji wa fedha za hazina ya vyama vya kisiasa

Fedha hizo zitagawanywa kwa njia zifuatazo—

(a) Asilimia 80 ya fedha za hazina hiyo kwa kuzingatia jumla ya kura ambazo chama hicho kilipata kwa uchaguzi mkuu uliotangulia;

(b) Asilimia 15 ya mgao wa fedha za hazina ya Vyama vya Kisiasa kwa mujibu wa idadi ya wagombeaji katika chama kutoka makundi maalumu waliochaguliwa katika uchaguzi mkuu uliopita; na

(c) Asilimia tano kwa usimamizi wa matumizi ya fedha za Hazina hiyo.

Kuhusu ugawaji wa fedha za hazina hii, idadi ya kura ambayo chama kimepata hupatikana kwa kuongeza kura zote zilizopigiwa chama katika uchaguzi mkuu uliopita katika wadhifa wa urais, wa ubunge, magavana na wawakilishi wa wadi.

## Vigezo vya kugawa fedha

Mwanzoni mwa mwaka wa matumizi ya fedha, Msajili atatoa notisi kwa vyama vyote ili kuvitaka vitume maombi ya fedha kutoka kwa Hazina ya Vyama vya Kisiasa kwa kuwasilisha stakabadhi zifuatazo:

(a) Mpangilio wa shughuli za chama husika cha kisiasa pamoja na muda wa kutekeleza shughuli hizo;

(b) Mpangilio wa kutoa kandarasi;

(c) Ripoti za matumizi ya fedha ambazo zimekaguliwa;

(d) Ripoti za kuonesha fedha zilizopokelewa na namna zilivyotumika;

(e) Fomu ya Chama cha Siasa Namba 15: Ambayo inaonyesha watu watakaoidhinisha kutolewa kwa fedha za chama kutoka kwa Hazina ya Vyama vya Kisiasa; na

(f) Fomu ya Chama cha Siasa Namba 16: Fomu ya kutuma maombi ya fedha kutoka kwa Hazina ya Vyama vya Kisiasa

Msajili wa vyama anaweza kuzuia kutolewa kwa fedha za vyama vya kisiasa ambavyo havizingatii mahitaji haya.

## Makosa juu ya chanzo cha fedha

Chama cha kisiasa ambacho kitapokea fedha kutoka kwa raia wa kigeni kinyume na mwongozo wa Sheria ya Vyama vya Kisiasa kitavunja sheria.

Sheria hii inakizuia chama cha kisiasa pamoja na mtu yeyote au muungano wowote kupokea na kugawanya fedha za kiwango fulani kwa chama cha kisiasa iwe ni pesa taslimu au ni bidhaa ambao

unazidi asilimia tano ya matumizi ya kijumla ya chama hicho kulingana na ukaguzi wa matumizi ya fedha ya chama hicho.

Chama cha kisiasa kinachopokea zaidi ya asilimia 5 ya fedha kinazotumia kulingana na ripoti ya ukaguzi wa fedha za matumizi ya mwaka uliotangulia kitakuwa kimevunja sheria na mbali na kuadhibiwa kulingana na Sheria aa Vyama vya Kisiasa, kitatatakiwa kuzitoa fedha hizo kwa serikali. Hata hivyo, Sheria hii haiwezi kutumika pale ambapo mwanzilishi wa chama ameamua kuchangia rasilimali za chama katika mwaka wake wa kwanza baada ya kuundwa.

Afisa wa chama cha kisiasa au mtu yeyote anayehitajika kuweka wazi mbele ya Msajili habari za fedha au raslimali nyinginezo za chama atakosa kutoa habari hizo kama inavyohitajika au anatoa habari za uongo kwa mujibu wa hazina hiyo au mali ambayo chama kimejipatia, basi atakuwa anavunja sheria na atatozwa faini ya pesa sawa na zile alizokosa kuzitolea habari au atahukumiwa kifungo kisichozidi miaka miwili gerezani au hukumu zote mbili kwa pamoja.

## Kuweka wazi habari za rasilimali, madeni na matumizi ya fedha katika shughuli za uchaguzi

Angalau katika kipindi cha siku sitini kabla ya uchaguzi, chama cha kisiasa kitawasilisha orodha ya majina ya wanachama wake pamoja na ripoti ya kuonyesha rasilimali yote ya chama kama ilivyoelekezwa kwenye fomu husika. Kulingana na Sheria hii, ni hatia kwa chama cha kisiasa kukosa kutimiza mahitaji ya kuwasilisha ripoti hii au kuwasilisha ripoti yenye habari za uongo.

## Ukaguzi wa akaunti za vyama vya kisiasa

Chama cha kisiasa kitahitajika kuweka rekodi na stakabadhi za fedha inazopokea, matumizi, raslimali na mali nyingine ya chama. Chama kitawasilisha ripoti ya matumizi ya fedha kwa Mkaguzi Mkuu wa fedha za umma kwa kipindi cha miezi mitatu baada ya mwaka wa matumizi ya fedha kukamilika.

Akaunti za chama cha kisiasa zitakaguliwa kila mwaka na Mkaguzi Mkuu wa fedha za umma na kisha ripoti itawasilishwa kwa Msajili ambaye ataiwasilisha ripoti hiyo kwa Bunge la Kitaifa.

Msajili anaweza wakati wo wote kumwomba Mkaguzi Mkuu wa Fedha za umma kuchunguza akaunti za chama chochote.

Mtu yeyote anakubaliwa kukagua ripoti ya ukaguzi wa akaunti zilizotolewa na chama baada ya kulipa ada inayotolewa kwa Msajili na hatimaye atapewa nakala za ripoti hiyo.

## Akaunti na ukaguzi wa matumizi ya fedha katika Afisi ya Msajili

Afisi ya Msajili itahitajika kuhifadhi rekodi na stakabadhi za kuonesha fedha zilizopokelewa, namna fedha hizo zilivyotumiwa pamoja na raslimali nyingineyo katika Afisi ya Msajili. Kwa kipindi cha miezi mitatu, baada ya mwaka wa matumizi ya fedha kukamilika, Afisi ya Msajili itawasilisha ripoti ya matumizi ya fedha ya ofisi yake pamoja na:

(a) Ripoti ya kuonesha fedha zilizopokelewa na namna zilivyotumiwa katika mwaka huo; na

(b) Ripoti ya rasilimali na madeni yaliyopo katika Afisi ya Msajili kwa kipindi hicho.

Akaunti zote zinazohifadhiwa kwa mujibu wa sheria hii zitakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa fedha za umma angalau mara moja kwa kipindi cha mwaka wa matumizi ya fedha.

## Michango

Vyama vya kisiasa vinakubaliwa kupokea michango ya aina yoyote. Kwa hakika, michango inaweza kusaidia ukuaji wa chama nchini Kenya na kukisaidia chama hicho kubuni na kutekeleza sera zake. Hata hivyo, michango hiyo inaweza kusababisha kuwepo kwa ushawishi usiofaa ili anayetoa michango hiyo aweze kufanya hivyo, kwa lengo la kufanikisha matakwa ya anayechangia na hivyo kuharibu maamuzi ya kibinafsi wakati waliochangiwa wako mamlakani. Ili kuepuka hili, Sharti wanaotoa michango pamoja na vyama vya kisiasa sharti vizingatie sheria. Sheria hii ndiyo inayounda kanuni zenyewe.

## Aina za mchango

Mchango unaweza kuwa mchango wa kifedha au mchango usiyo wa kifedha.

## Mchango wa kifedha

Mchango wa fedha ni kiwango cha pesa taslimu zinazotolewa na hazihitaji kulipwa.

## Mchango usio wa kifedha

Mchango usio wa kifedha ni gharama ya huduma au mali au matumizi ya mali au pesa hivi kwamba ni kama kimetolewa bure au kwa gharama ya chini mno.

## Wanaofaa kuchangia

Sharti michango, misaada, urithi na ufadhili utoke kwa watu au makundi yanayokubaliwa kisheria. Ni sharti vyama vya kisiasa vijifahamishe na sheria zingine zinazoweza kutoa mwongozo kuhusu suala hili kama vile sheria ya inayohusu mali itokanayo na uhalifu na ulanguzi wa fedha.

Ni mwananchi wa Kenya peke yake anayetambuliwa na katiba na yule anayetambuliwa na sheria ya uhamisho pekee ndiye aliye na ruhusa ya kutoa mchango kwa chama cha kisiasa.

Wakati chama kinapopokea mchango usio wa kifedha kutoka kwa mtu binafsi, sharti kipatestakabadhi kamili za gharama za bidhaa au huduma zilizotolewa kwa njia ya mchango pamoja na jina na habari za mawasiliano za anayetoa mchango huo.

Kundi la kigeni au chama cha kisiasa kutoka nchi ya kigeni ambacho kinakubaliana na sera za chama cha kisiasa ambacho kimesajiliwa nchini Kenya linaweza kutoa msaada wa kitaaluma bali sio mchango wa rasilimali kwa chama. Msaada wa kitaaluma hautajumuisha kutolewa kwa rasilimali zozote kwa chama cha kisiasa.

### Kukubali mchango

Mchango wa kifedha unasemekana kuwa umekubaliwa pindi baada ya kupokelewa na chama cha kisiasa. Mchango usio wa kifedha unasemekana kuwa umekubaliwa wakati chama cha kisiasa kinaporuhusu kutumiwa kwa rasilimali au kupokea huduma husika.

### Kiwango cha mchango

Sheria haijaweka wazi kiwango cha fedha zinazofaa kutolewa kama mchango.

### Mchango usiofaa

Ifuatayo ni aina ya michango isiyofaa, iwe kwa namna ya fedha au namna isiyo ya fedha:

(a) mchango kutoka kwa watu wasio wananchi wa taifa la Kenya;

(b) mchango kutoka kwa mataifa ya kigeni; na

(c) mchango kutoka kwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali.

## SURA YA 10: MAHITAJI YA KUTOA RIPOTI

Sehemu hii ina habari za kijumla kuhusu yanayohitajika wakati wa kutoa ripoti za matumizi ya fedha na zile zisizohusu masuala ya fedha za vyama vilivyosajiliwa kwa kipindi cha mwaka mzima au zinazohusu masuala muhimu ya uchaguzi mkuu na uchaguzi mdogo.

Katibu mkuu wa chama kilichosajiliwa ana jukumu la kusimamia shughuli zote za kifedha na kuwasilisha ripoti inayohitajika kwa mujibu wa sheria.

### Ripoti ambayo haihusu fedha

#### Mabadiliko ambayo sharti msajili wa vyama vya kisiasa afahamishwe

Wakati ambapo chama cha kisiasa ambacho kimesajiliwa kikamilifu kinataka kubadilisha au kufanyia marekebisho—

(a) Katiba yake;

(b) kanuni na mwongozo wake;

(c) anwani  jina au habari za mawasiliano za kiongozi yeyote wa chama cha kisiasa;

(d) jina lake, alama, kauli mbiu, rangi; au

(e) anwani na mahali palipo na afisi za makao makuu,

Msajili anafaa kujulishwa kuhusu mabadiliko ya aina yoyote ili achapishe ombi hilo kwenye Gazeti Rasmi la Serikali katika kipindi cha siku 14 baada ya kupokea ombi la chama.

Baada ya siku kumi nne tangu kuchapishwa kwa ombi la mabadiliko kwenye Gazeti Rasmi la Serikali, chama cha kisiasa kinaweza kufanyia katiba au kanuni zake mabadiliko kwa kuzingatia maoni ya wahusika. Baada ya siku kumi na nne zingine, chama cha kisiasa sharti kimfahamishe Msajili kuhusu uamuzi uliochukuliwa na mabadiliko yaliyofanyiwa yaliyofanywa katiba na kanuni zao.

Hatimaye chama cha kisiasa kinahitajika kuchapisha mabadiliko hayo kwenye magazeti mawili makuu ya humu nchini yenye usambazaji wa kitaifa.

### Mabadiliko ya viongozi waliochaguliwa

Sheria inawatambua “viongozi waliochaguliwa” kuwa viongozi wowote wa chama waliochaguliwa au kuteuliwa na chama cha kisiasa kwa mujibu wa katiba ya chama husika. Kiongozi wa chama kilichosajiliwa anapoondoka ofisini au kuingia ofisini, chama cha kisiasa kitamfahamisha Msajili katika kipindi cha siku 30.

### Notisi ya kubadilishwa kwa sehemu au anwani ya afisi za makao makuu

Chama kitamfahamisha Msajili katika kipindi cha siku kumi na nne kuhusu mabadiliko ya sehemu au anwani ya afisi za makao makuu baada ya kufanya mabadiliko hayo.

## Kuripoti kuhusu masuala ya fedha

### Baada ya kusajiliwa

Katika kipindi cha siku 60 baada ya kukabidhiwa cheti za usajili rasmi, chama cha kisiasa kinahitajika kumkabidhi Msajili wa Vyama vya Kisiasa tangazo lililoandikwa la kuonesha rasilimali zote na fedha zote za matumizi ikiwa ni pamoja na michango, misaada ziwe pesa taslimu au usaidizi wowote ambao ulitolewa au unatarajiwa kutolewa kama rasilimali za mwanzo za chama cha kisiasa kutoka kwa wanachama waanzilishi kwa siku sitini za kwanza katika mwaka wa kwanza.

Tangazo hilo sharti—

(a) lioneshe zilikotoka fedha na raslimali za chama cha kisiasa;

(b) liwe na habari zote kama zinavyotakiwa na Msajili ; na

(c) liambatane na tangazo la kisheria lililofanywa na mtu ambaye ameteuliwa na uongozi wa chama cha kisiasa kutoa tangazo hilo.

Msajili anatakiwa kuchapisha tangazo hilo kwenye gazeti rasmi la serikali na kwa angalau gazeti moja kuu nchini lenye usambazaji wa kitaifa katika kipindi cha siku 30 baada ya kulipokea. Msajili anaweza kukifutilia mbali chama cha kisiasa ambacho hakitawasilisha tangazo hili la kuweka wazi utajiri wake au kutoa habari za uongo kuhusu jambo hili.

### Ripoti ya kifedha ya kila mwaka

Katika kipindi cha siku tisini baada ya kukamilika kwa mwaka wa matumizi ya fedha ambao sharti uwe mwaka wa kifedha wa kiserikali, chama cha kisiasa sharti kichapishe habari hizi kwa magazeti mawili makuu nchini ambayo yanafika kila pembe ya taifa:

(a) Mahali ambapo fedha zake zimetoka;

(b) Fedha kilizopokea na kilizotumia; na

(c) Rasilimali na madeni yake.

### Kuhusu uchaguzi

Vyama hupokea na hutumia rasilimali zake nyingi wakati wa uchaguzi. Ili Msajili ahakikishe kuwa vyama vyote vya kisiasa vimeendesha uteuzi na uchaguzi wa haki na uwazi katika kipindi cha uchaguzi, ni muhimu kwa kila chama kuweka wazi rekodi zake kwa wakati kwa ajili ya ukaguzi. Kwa hivyo, kkatika kipindi cha angalau siku tisini kabla ya uchaguzi mkuu, chama cha kisiasa kitawasilisha majina ya wanachama na taarifa kuhusu rasilimali na madeni ya chama.

### Ukaguzi wa akaunti na matumizi ya fedha

Hazina hii inafadhiliwa na pesa za watoa ushuru, na hivyo basi lazima matumizi yake yachunguzwe ili kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa zinatumika kulingana na malengo yalizo tengewa. Katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kila mwaka wa kifedha, chama cha kisiasa kitawasilisha ripoti ya matumizi ya fedha kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za umma ya akaunti yake. Mkaguzi wa serikali atakagua kisha awasilishe ripoti ya ukaguzi wake kwa Msajili ambaye hatimaye ataiwasilisha ripoti hiyo kwa Bunge la Taifa.

## SURA YA KUMI NA MOJA: KANUNI ZA MAADILI ZA VYAMA VYA SIASA

Kwa mujibu wa Katiba, chama cha siasa kinawajibika kuzingatia mahitaji baadhi yake yakiwa kufuata kanuni za kimaadili za vyama vya kisiasa.  Kabla ya chama cha kisiasa kukabidhiwa

cheti cha usajili kamili lazima kijitoe kuzingatia Sheria ya Vyama vya Kisiasa 2011 na Kanuni za Maadili ambazo zinaelezwa kwenye Sheria.

Kanuni za Maadili ni mkusanyiko wa kanuni ambazo hueleza majukumu ama utendaji ufaao wa mtu binafsi, chama ama shirika.  Kanuni hii inahitaji vyama vya siasa kujitoa kuzingatia mahitaji yake.  Inaelekeza mienendo ya wanachama na wale wenye vyeo vya uongozi kwenye chama, wale wenye nia ya kuania vyeo, wagombea na wafuasi wao kwa lengo la kukuza uongozi mwema na kuangamiza matendo maovu ya kisiasa.

Kanuni hii ina lengo kudhibiti ushindani wa kisiasa na ushirikiano kwa misingi ya sheria na maadili mwafaka yanayokubalika ulimwenguni. Kanuni inahitaji vyama:-

(a) Kukuza sera mbadala ambazo zinaafikiana na matarajio, hofu na matakwa ya wananchi wa Kenya
(b) Kuheshimu na kuzingatia mchakato wa demokrasia wakati wanapong'ang'ania nguvu za kisiasa ili waweze kutekeleza sera zao.
(c) Kukuza ukubaliano wakati wa kuunda sera ya uamuzi juu ya maswala yenye umuhimu wa kitaifa.
(d) Kuunda na kutekeleza mikakati ya kimaendeleo ya kufikia uwakilishi na ushiriki wa makundi maalum katika vitengo vya uongozi;na
(e) Tekeleza mradi wa kuleta usawa, sera na mipango mikakati juu ya uwakilishi wa kisiasa kwa mujibu wa Katiba.

Kila chama cha kisiasa kinahitajika:

(a) Kuheshimu haki za watu wote kushiriki katika mchakato wa kisiasa yakiwemo makundi ya watu wenye mahitaji maalumu.
(b) Kuheshimu na kukuza usawa wa kijinsia, haki za kibinadamu na uhuru wa kimsingi;na
(c) Kuwa na uvumilivu na ushirikishi katika matendo yao yote ya siasa.

Zaidi ya hayo, chama cha kisiasa kinahitajika;

(a) kuheshimu, kuzingatia na kulinda Katiba ya Kenya;
(b) kuheshimu na kulinda Sheria hii na sheria nyingine ye yote ambayo imeandikwa kuhusiana na uchaguzi na vyama vya kisiasa;
(c) kuheshimu, kuzingatia na kulinda Katiba,  kanuni za uchaguzi za chama na kanuni zingine zo zote cha chama ambazo zimeundwa na kuidhinishwa kwa mujibu wa kanuni hizi za maadili;
(d) kuheshimu, kuzingatia na kukuza hadhi ya utu, usawa, haki ya kijamii, ushirikishi na kutobagua na kulinda waliotengwa;
(e) kuheshimu, kuzingatia na kukuza haki za binadamu na kutii  sheria

(f) kukuza uzalendo na umoja wa kitaifa
(g) kuheshimu, kuzingatia na kukuza maadili ya kidemokrasia na misimamo yake, kuhakikisha ushirikishi wa wanachama na uwakilishi ufaao katika uongozi kwa ajili ya maendeleo ya nchi;
(h) kuheshimu, kuzingatia na kukuza uongozi mwafaka, uadilifu, heshimu, uvumilivu, uwazi na uajibikaji.
(i) kukuza ushirikiano katika ushindani wa kisiasa
(j) kukuza mgawanyo na ugatuzi wa mamlaka na rasilimali;
(k) kuheshimu, kuzingatia na kukuza tabia za kidemokrasia kwa kuwa na uchaguzi wa mara kwa mara ambao utakuwa huru, wa haki na kuaminika katika chama na isitoshe wawe na viongozi ambao wamechaguliwa kidemokrasia kuongoza vitengo mbalimbali vya chama.
(l) kuheshimu, kuzingatia na kukuza tabia za kidemokrasia kwa kuendesha uteuzi huru, wa haki na wa kuaminika;
(m) kuheshimu, kuzingatia na kukuza uongozi na uadilifu kwa mujibu wa Katiba ya Kenya; na
(n) kuendesha shughuli zake kwa uwazi na uajibikaji katika kutunga sheria, kanuni, vitengo, mikakati na utendaji.

Chama cha kisiasa hakiruhusiwi:

(a) kujiingiza ama kuchochea vurugu miongoni mwa wanachama ama waafuasi wake;
(b) kujiingiza ama kuhimiza aina ye yote ya vitisho dhidi ya wapinzani wao ama mtu mwingine yo yote ama chama kingine cha siasa;
(c) kujiingiza kwenye vitendo vidogo visivyokuwa muhimu, kutoa hongo ama aina nyingine ye yote ya ufisadi;
(d) kutumia pesa ambazo zimepatikana kwa njia isiyofaa;
(e) kutumia mali ya umma isipokuwa ile imetolewa kuwa matumizi ya vyama vya kisiasa kupitia kwa hazina ya vyama vya siasa;
(f) kuhimiza matumizi ya chuki ambayo yaweza kuleta uhasama wa kikabilia, kueneza chuki dhidi ya wengine ama kuhamasisha watu kuumiza wengine;
(g) kuzuia, kuharibu ama kuiingilia kwa njia ye yote ile mikutano, hadhara ama maandamano ya chama kingine cha kisiasa ama uongozi wake;
(h) kuanzisha ama kudumisha kikundi cha kijeshi, kigaidi ama shirika lingine lo lote ama kuwa na uhusiano na shirika kama hilo;
(i) kutumia mali ya taifa kufanya kampeni za mapendeleo.

Chama cha siasa kitakuza uhusiano kati ya vyama vya siasa kwa:

(a)kuhakikisha kuwa kuna ushindani miongoni kwa vyama kwa kuzingatia mielekeo na kanuni, tofauti;
(b) kupalilia uaminifu na uhakiki kupitia mikakati ya ushirikiano;

(c) kudhibiti na kuzuia tofauti za kisiasa kwa majadiliano na kujenga upatano miongoni mwa vyama vya siasa;na
(d) Kukuza maridhiano ya kitaifa na kujenga umoja wa kitaifa.

## Matokeo ya kutozingatia kanuni za maadili

Mtu hawezi kuwa mwanachama wa chombo tawala cha chama cha kisiasa iwapo mtu huyo ameondolewa kwa kipindi cha miezi sita kwa ajili ya kutozingatia Kanuni za Maadili za chama cha siasa. Kuenda kinyume na Kanuni za Maadili kunaweza kusababisha kufutwa kwa usajili wa chama cha kisiasa.

## Makosa na adhabu

Ni makosa mtu kukosa kutoa mambo fulani ama arifa inayohitajika kutolewa na chama cha kisiasa kwa mujibu wa Sheria ama kutoa kauli ambayo mtu anajua kuwa ni uwongo kuhusu chama cha kisiasa na hana sababu ya kuamini ni kweli.

Ni makosa pia mtu kudidimiza ama kujaribu kudidimiza kitendo cha siasa cha mtu ambacho ni halali kisheria na akihukumiwa atahitajika kutoa faini isiyozidi shilingi milioni moja ama kufungwa kwa kipindi kisichozidi miaka miwili ama yote mawili.

Pale ambapo chama kimefanya kosa kwa mujibu wa Sheria, kila Afisa mkuu wa chama hicho atachukuliwa kuwa ndiye ametenda kosa.

Mtu ambaye amehukumiwa kwa ajili ya kufanya kosa kwa mujibu wa Sheria ambapo adhabu haijabainishwa, baada ya kuhukumiwa, atatozwa faini ya shilingi zisizozidi milioni moja ama kufungwa kwa kipindi kisichopungua miaka miwili ama yote pamoja.